# Nipashe

Jumatano Septemba 18, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581803
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US


NDIVYO WAGOMBEA URAIS MAREKANI WALIVYOCHUANA
siasa
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Wasomi wanavyomwunga mkono Rais wakihubiri nishati safi, ulinzi hifadhi
MAUAJI NA UKATILI UNAOENDELEA...
Imetimu wakati wa kuanza kutumia Mahakama ya Korona
• Iko kisheria, japo wengi hawaifahamu
UKURASA 11

**Mtoto** wa miaka sita alivyoomba msaada mauaji ya watu watatu
UKURASA WA 3

**Rais** Mwinyi awakaribisha wawekezaji filamu, utalii
UKURASA WA 3



**Hospitali** yaamriwa kulipa bilioni 1.3/- NSSF za watumishi
UKURASA WA 8

## UTEKAJI, MAUAJI

# Samia avunja ukimya

• **Polisi** nao awapa angalizo lao... *Endelea Ukurasa 2*



Gwaride la heshima lililoandaliwa na Jeshi la Polisi likipita mbele ya Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Dk. Samia Suluhu Hassan wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 60 ya jeshi hilo, katika Shule ya Polisi Tanzania (TPS), Moshi, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: IKULU**

## Ukubwa wa Deni la Taifa...

# Kuna sababu Watanzania kutaharuki?

**Na Ludovick Utouh**

UKUAJI wa Deni la Taifa unapaswa uendane na ukuaji wa uchumi wa nchi ili deni hilo liwe himilivu.

Wananchi wana haki ya kujua madhumuni ya mikopo inayochukuliwa na serikali na wana haki ya kujihakikishia kuwa mikopo inayochukuliwa na serikali inatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa...

ENDELEA UK. 4 & 5



Baadhi ya maaskofu na wakuu wa jimbo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Askofu wa Dayosisi ya Mwanga, Chediel Sendoro (54), kabla ya maziko yake, katika Kanisa Kuu la Mwanga, mkoani Kilimanjaro jana. **PICHA: MARY MOSHA**

# Malasusa aungana na wadau, vilio vya utekaji na mauaji

UKURASA 2

**MICHEZO** RAIS CAF ATOA KAULI MECHI SIMBA LIBYA UK.24

**MAONI,** UK.6

# Malasusa aungana na wadau vilio vya utekaji, mauaji

**Na Waandishi Wetu,** MWANGA

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Alex Malasusa, amesema matukio ya kutekwa au kutoweka kwa Watanzania ambayo hayakuzoeleka na yanayoendelea hivi sasa, yanapaswa yafike mwisho.

Pia, amemuomba Naibu Waziri Mkuu, Dk. Dotto Biteko, kufikisha salaam za kanisa hilo kwa viongozi wakuu wa nchi kuruhusu kuwapo na meza ya majadiliano ili kupatikane suluhisho la hayo mauaji.

Askofu Dk. Malalsusa, alitoa ujumbe huo wa KKKT jana katika Kanisa Kuu la Usharika wa Mwanga, wakati wa ibada ya maziko ya aliyekuwa Askofu wa Dayosisi ya Mwanga, Dk. Chediel Sendoro, aliyezikwa katika Kanisa Kuu la Usharika wa Mwanga.

Askofu Dk. Chediel Sendoro, alipoteza maisha Septemba 9, mwaka huu kwa ajali majira ya saa 1:30 usiku, baada ya gari alilokuwa akiendesha kugongana uso kwa uso na lori eneo la Kisangiro, wilayani Mwanga.

Dk. Chediel Sendoro, ni mtoto wa Askofu wa kwanza wa Dayosisi ya Mashariki na Pwani, Dk. Elinaza Sendoro.

Akizungumzia matukio ya utekaji na kutoweka kwa Watanzania, Dk. Malasusa alisema, "Nimepata fursa ya kutamka masikitiko yetu, hasa kwa hali inayoendelea katika nchi yetu kwa kusikia habari ambazo sio nzuri.

Vifo, utasikia habari nyingi sana katika kipindi hiki, hasa katika barabara zinazounganisha nchi yetu na hakika sisi sote tukichukua wajibu wetu, basi huenda tukavifuta au kuvipunguza.

"Lakini samabamba na hilo, masikio yetu na mengine yameshuhudia jinsi ambavyo tumekuwa na matukio ambayo hayakuzoeleka, hasa tukitumia maneno yanayotumika sasa 'kutekwa' au 'kutoweka' kwa Watanzania.

Nafikiri tuseme hivi ifike mwisho, kanisa liombe kwa ajili ya jambo hilo. Na mauaji ndugu zangu, Biblia iko wazi kabisa, nchi inalaaniwa damu inapomwagika. Hatutaki laana iingie katika nchi yetu, tuombe kila mwenye kujua maana ya maombi kuliombea jambo hili; najua wanasiasa wamekuwa wakilizungumza, lakini hebu tulisogeze pia kama haja yetu mbele za Mungu.

"Nachukua fursa hii kuomba Jumapili zijazo wachungaji, maaskofu katika kanisa letu tuanze kuomba kama kitu cha pekee kilichotokea katika nchi yetu.

Naibu Waziri Mkuu (Dk. Dotto Biteko), niwasihi kama raia, kama kiongozi wa imani, wanasiasa kuruhusu kuwapo na meza ya majadiliano, huenda likapatikana suluhisho la haya mauaji."

Kadhalika, Askofu Dk. Malasusa, alisema hivi sasa imekuwa tabia na hata wengine wanauawa, kwa sababu watu wanaonekana wanaiba watoto, wengine wamekuwa wakipigwa na mambo kadhaa wa kadhaa, hivyo ni vyema kuweka muda wa kuzidi kusikilizana.

Kutokana na yanayoendelea, Dk. Malasusa amewaelekeza maaskofu wa KKKT, kama wanajua wana kitu, mawazo wasiache kuyatoa. Tumefika katika kipindi ambacho Watanzania wamekuwa na hofu.

**AJALI ILIVYOKUWA**

Kamanda Maigwa, alisema kabla ya kupoteza maisha, Askofu Sendoro na mwanawe ambaye anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, alikuwa akitokea katika mji mdogo wa Himo, Wilaya ya Moshi kwenda Mwanga.

Alisema gari lake lilikuwa likiyapita magari mengine mawili na kisha kugongana uso kwa uso na lori lililokuwa likitokea Tanga kwenda mkoani Arusha.

**MAISHA YAKE**

Askofu Sendoro, ambaye hadi anafariki dunia alikuwa mhitimu wa Shahada ya Uzamivu (PhD) na Shahada ya juu ya Uhasibu (CPA), alizaliwa Mei 1, 1970 akiwa mtoto wa nne wa Askofu Dk. Elinaza Sendoro.

***Imeandikwa na Godfrey Mushi na Mary Mosha (Mwanga).**



Katibu Mkuu wa Chama cha NLD, Doyo Hassan (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana wakati akitoa tamko la kupinga maandamano yaliyoitishwa na baadhi ya vyama vya siasa. Katikati ni Mwenyekiti wa Umoja wa Vyama 13 visivyokuwa na wawakilishi bungeni, Abdul Mluya na Mwenyekiti wa Chama cha Sauti ya Umma, Bertha Mpata. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Samia avunja ukimya utekaji, mauaji

**Elizabeth Zaya na Godfrey Mushi**

RAIS Samia Suluhu Hassan rasmi amevunja ukimya, akiwa na ufafanuzi wake kuhusiana na madai dhidi ya serikali juu ya matukio ya utekaji na mauaji ya watu.

Sambamba na hilo, Rais amelielekeza Jeshi la Polisi katika maeneo manne yanayogusa ufanisi wa utendaji wake, akioanisha na madai yanayoendeleza kuelekezwa kwalo.

Mkuu wa Nchi aliyasema hayo jana kwenye Shule ya Polisi Tanzania (TPS) iliyoko Moshi, mkoani Kilimanjaro, ambako alishiriki Maadhimisho ya Miaka 60 ya jeshi hilo, akifunga mkutano mkuu wa mwaka wa maofisa waandamizi, makamanda wa mikoa na vikosi.

Rais aliagiza wizara na jeshi hilo kuendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume ya Haki Jinai kwa ukamilifu na kuendelea kutekeleza mapendekezo yote yasiyohitaji mabadiliko ya sheria au ongezeko kubwa la bajeti.

Aliagiza Jeshi la Polisi kama walinzi wa raia na mali zao ambalo lina haki ya usimamizi wa haki na sheria, halipaswi kuhusishwa au kuhisiwa kwa namna yoyote katika tuhuma za ukiukwaji wa sheria na haki linazosimamia.

Rais alielekeza jeshi hilo liongeze kasi ya matumizi ya Tehama ili lidhibiti uhalifu na wahalifu kwa ufanisi zaidi.

Vilevile, alielekeza wizara kutekeleza maelekezo ya serikali kuhakikisha mifumo inasomana na taasisi nyingine.

Mkuu wa Nchi alionesha kukerwa na matukio ya mauaji na utekaji watu yanayoendelea kuripotiwa nchini, akitaka jamii kutofumbia macho vitendo hivyo kwa kushindwa kutoa taarifa na kusubiri kulaumu jeshi kutoa matamko na kulaani.

Alisema serikali inazo taarifa kuhusu njama zinazopangwa na baadhi ya watu wanaoendesha mipango ya uvunjifu wa amani, akionya kuwa serikali haitawavumilia.

"Tumeshuhudia mauaji ya watu wazima na watoto kwa imani za kishirikina kama ilivyoibuliwa na Jeshi la Polisi hivi karibuni, kumekuwa na matukio ya wapenzi kuuana, wazazi kuua watoto na watoto kuua wazazi wao kikatili na kisha maiti kuchomwa moto na wengine kukatwa vipande na kufufukiwa, na mambo ya aina hiyo ambayo kwa vyovyote vile hayaridhishi.

"Huku ni kuondokwa na utu na ni uhalifu mkubwa sana, wananchi wanakata tamaa kuona matukio haya yanahusishwa si tu na waganga wa kienyeji, bali hata watu mashuhuri kama viongozi wa dini na hata wazazi na watoto," alisema.

Akizungumzia tukio la kuuawa kwa kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Ali Kibao lililotokea hivi karibu, Rais Samia alisema serikali ilisikitishwa na jambo hilo na kutoa maelekezo kwa vyombo vya dola.

"Kifo hicho kimeleta hisia kali pia kwa wawakilishi wa baadhi ya mataifa ya nje na wawakilishi wa nchi zao hapa kwetu. Ninataka niungane nao na niseme kwamba kwa sababu yoyote ile, mauaji haya hayakubaliki na ndio maana serikali tuliyalaani na kutaka uchunguzi wa haraka ufanyike na ndivyo inavyofanyika duniani kote.

"Baada ya mambo haya kutokea, serikali husimama kulaani na kutaka vyombo vyake vya usalama kwenda na uchunguzi na tujue kilichotokea na kazi hii nimeambiwa inaendelea vizuri," alisema.

Aliendelea: "Niseme tu kwamba baada ya tukio lile, nimekuwa nikiangalia maoni ya viongozi mbalimbali wa kisiasa, viongozi wa dini na baadhi wakiniomba nikemee mambo hayo.

"Maoni ya wazee mashuhuri, nimemsikia Mzee Butiku naye kasema, wawakilishi wa mataifa ya nje hapa nchini nao wametoa matamko, jumuiya za kiraia na wananchi kwa ujumla nao wamesema waliyoyasema.

"Hisia za makundi yote niliyoyataja, zikiibuliwa na kifo cha mtu mmoja tu niliyemtaja, ndugu yetu Ali Kibao, lakini kuna vifo vinasemwa muda baada ya muda, watoto albino wanakatwa mikono, wanauliwa, watoto wadogo wanachukuliwa, wanakatwa sehemu nyeti wanatupwa, sijui nani wanauliwa.

"Mpaka leo (jana) asubuhi nimepewa ripoti huko Dodoma watu watatu wamekutwa chumbani wameuliwa, lakini yanapotokea haya kwenye maeneo yetu lakini kuko kimya mpaka polisi iibuke iseme, wengine hawasemi.

"Hii inashangaza kwamba kifo cha ndugu yetu Kibao, kimeibua wimbi kubwa kulaani, kusikitika, kulaumu, kuita serikali ya wauaji, hii si sawa," Rais Samia alitamka kwa hisia kali.

Mkuu wa Nchi alisema, "Nilikuwa nasikiliza kwa makini, maelezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, nimerushiwa na nimeisikiliza vizuri sana clip ya Dk. Slaa wa CHADEMA, vilevile clip ya Joseph Yona wa Chalinze, wote wakitoa mipango ya taswira ya uvunjifu wa amani inayopangwa na baadhi ya vyama vya siasa.

"Nayaunganisha haya na uamuzi wa kikao cha Septemba 11 mwaka huu kilichofanywa na chama kimoja cha siasa kule Ngurelo, mkoani Arusha, ambacho kimeazimia kuwatumia na kuwachochea vijana kwa kuzusha tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, kufanya siasa chonganishi kwenye misiba na kushusha morali kwa jeshi hilo ili washindwe kufanya kazi yao ya kulinda usalama wa raia na mali zao."

Rais Samia pia alitunuku vyeti vya pongezi kwa askari polisi wastaafu 10 wa kwanza kabla na baada ya uhuru, waliotumikia jeshi hilo kwa uzalendo, uhodari na uajasiri hadi walipostaafu kwa heshima.

Kati ya askari hao wastaafu, wamo ambao walikuwa miongoni mwa askari wanane wa kwanza wa kike waliojiunga na kuajiriwa katika Jeshi la Polisi Tanganyika mwaka 1958.

Pia yumo askari wa kike ambaye ni miongoni mwa askari wa kike 12 wa kwanza kuajiriwa na Jeshi la Polisi Zanzibar baada ya Mapinduzi Matukufu.

HABARI KITAIFA

## Mwinyi awakaribisha wawekezaji utalii, filamu ndani ya Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema Zanzibar bado inahitaji wawekezaji zaidi kwa kuwa kuna maeneo mengi yenye fursa ambayo hayajafikiwa na kutangazwa kimataifa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Mawsiliano, Ikulu, Zanzibar, Dk. Mwinyi alisema hayo jana alipokutana na timu ya wawekezaji kutoka bara la Asia waliofika kueleza lengo la ujio wao kwa Zanzibar. Rais Mwinyi alikutana na wawekezaji hao Ikulu, Zanzibar.

Aliwahakikishia wawekezaji hao kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itawapa ushirikiano wa kutosha na kufungua milango mipya ya uwekezaji na kudumisha ushirikiano.

Rais Mwinyi aliyataja maeneo yanayohitaji uwekezaji zaidi kuwa ni pamoja na utalii wa mikutano, michezo, utalii wa afya na utalii wa matamasha na kuwahimiza wawekezaji hao wafanye utekelezaji wa haraka wa dhamira yao kwa kuwa serikali iko tayari kufanikisha azma zao.

Kuhusu kilimo cha viungo vya asili vya Zanzibar, Rais Mwinyi alisema ni eneo muhimu ambalo serikali inalipa kipaumbele na kuwashauri wawekezaji hao kuliangalia kwa karibu kutokana na Zanzibar kuwa na utajiri wa bidhaa hizo ambazo bado hazijaingia kwenye soko la Asia.

Eneo lingine ambalo aliligusia ni la uandaaji wa filamu ambalo India imefanikiwa kwa kiasi kikubwa na kuwasisitiza kuangalia uwezekano wa kutoa mafunzo kwa waandaaji wa filamu wazalendo na pia kuwaleta wasanii mashuhuri wa India kuandaa filamu zao nchini.

Alisema Zanzibar inahitaji kuwa na hoteli za daraja la juu zaidi akitolea mfano wa hoteli ya Taj iliyoko India, kujengwa Zanzibar huku akiwahakikishia serikali imejipanga vizuri dhidi ya vikwazo vyovyote ili kufanikisha jambo hilo.

Akizungumza katika kikao hicho, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema wizara imezungumza na timu ya wawekezaji hao kuhusu kuitangaza Zanzibar kwenye ukanda wa bara la Asia na kutafuta soko la uhakika la bidhaa zinazozalishwa nchini.

Naye Mratibu wa ugeni huo, Rajiv Desai, ambaye ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Utalii ya 'Swahili Safari' alisema kampuni yake imeandaa mkakati maalum wa kuwaunganisha wawekezaji kutoka Dubai na India kuwekeza Zanzibar kutokana na kuvutiwa kwa maumbile ya kijiografia yenye ushawishi wa utaalii na ukarimu wa Wazanzibari.

Katika hafla hiyo, lilizinduliwa jarida la 'BlitzIndia' lenye nia ya kuitangaza Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kimataifa kwenye nyanja za uchumi, maendeleo, utalii, sanaa na utamaduni. Rais Dk. Mwinyi alikabidhiwa nakala ya jarida hilo lililozinduliwa rasmi Ikulu.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akizungumza na ujumbe wa wafanyabiashara mbalimbali kutoka nchini India, ukiongozwa na Rajiv Desai (kulia kwa Rais), Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Mtoto wa miaka sita alivyoomba msaada watu watatu wakiuawa

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi mkoani Dodoma limeeleza mtoto mwenye umri wa miaka sita alivyoomba msaada katika tukio la mauaji ya watu watatu Mtaa wa Segubwawani, Kata ya Nala, jijini Dodoma.

Akizungumzia tukio hilo lililotokea juzi, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Anania Amo alisema kuwa watu hao walikutwa wamefariki dunia huku mama mwenye nyumba akijeruhiwa na watu wasiojulikana.

Alisema kuwa katika tukio hilo, hakuna jirani ambaye alisikia kelele, bali mtoto aliyetumwa kwenda katika familia hiyo kufuata redio waliyoazima, alirudisha habari kuwa hakupata ushirikiano.

Kamanda Amo alisema kuwa kutokana na hali hiyo, majirani walikwenda katika nyumba hiyo na kusikia sauti ya mtoto wa miaka sita ambaye alikuwa katika nyumba hiyo akipiga kelele kuomba kufunguliwa mlango.

"Mtoto huyo hajajeruhiwa, ndiye alipiga kelele, akiomba kufunguliwa maana milango ilikuwa imefungwa. Ndipo baadaye waligundua kuwa kuna mauaji yamefanyika," alisema.

Alifafanua kuwa waliouawa ni watoto wawili wa familia moja ambao miili yao imekutwa imeungua moto huku mfanyakazi wa ndani, akikutwa na majeraha kichwani.

Kamanda Amo alisema kuwa mama alijeruhiwa, aliwahishwa hospitalini kupata matibabu.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Segubwawani, Kata ya Nala, Jeremia Molima alisema alipewa taarifa ya tukio hilo juzi saa 9.45 alasiri na alipofika katika eneo hilo alikuta watu wanaingia ndani na kuwaomba watoke, wasubiri askari polisi wafike.

"Baada ya kufika, nilikuta watoto wawili wameungua kwa moto, halafu kuna dada wa kazi amelala kifudifudi amekufa, anaonekana kichwa chake kimeshambuliwa kwa sababu kwenye sakafu na damu imeganda.

"Tumemkuta mama mwenye nyumba akiwa hoi, ameshambuliwa, alikuwa akitamka kuwa anajihisi maumivu, anaomba akalale," alisema.

Alisema kuwa walichokifanya ni kumwita bodaboda kwa ajili ya kumwahisha katika Zahanati ya Nala kwa ajili ya huduma ya kwanza na wakati wakiwasiliana na askari polisi kata ambaye aliwaeleza kuwa alikuwa njiani akielekea eneo la tukio.

Molima alisema kuwa baba wa familia aliyemtambulisha kwa jina la Robert Mgema, ni mwalimu mkoani Singida, hivyo katika nyumba hiyo walikuwa wanaishi mama, watoto wake watatu na mfanyakazi wa ndani.

"Juzi hapa walikuwa na sherehe ya mtoto aliyemaliza darasa la saba (mmoja kati ya waliouawa), hivyo baba wa familia alifika katika sherehe ya kumpongeza mtoto wao na haikufahamika wakati tukio linatokea kama alikuwa amesharejea katika kituo chake cha kazi au la.

"Inaelekea watu waliwavamia, wakawapiga hadi kuwaua, lakini hawa watoto wawili walioungua ndio tunashindwa kupata majibu ya haraka," alisema.

Kiongozi huyo alisema kuwa hakuna dalili ya moto kuwaka muda wa karibuni na hivyo wanahisi kuwa tukio hilo lilifanyika usiku.

Aliongeza kuwa Jumamosi walipokuwa na sherehe ya mtoto wao ya kumaliza darasa la saba, walikwenda kuazima redio kwa jirani kwa ajili ya sherehe.

"Leo (jana), mwenye redio alimtuma mtoto mdogo kwenda kuifuata lakini alipofika alikuta milango yote imefungwa, pamepoa na hakuna mtu anayeitika.

"Alirudi nyumbani kuwaeleza hali hiyo, ndipo majirani wakaenda. Lakini ndani ya nyumba kulikuwa na mtoto mdogo (ambaye hakuguswa), baada ya kuita kwa muda ndipo mtoto aliitika na kusema anaogopa kufungua mlango," alisema.

Alisema kuwa ndipo walipofungua wenyewe kwa nje na kuingia ndani na kukutana na mauaji hayo huku nguo zikiwa zimevurugwa, ziko chini na televisheni iko ukutani na haijaguswa kwa lolote.

Kwa mujibu wa Kamanda Amo, waliouawa ni Milcah Robert (12) aliyehitimu darasa la saba Shule ya Msingi Chihoni, Fatuma Mohamed (20) na dada wa kazi aliyetambulika kwa jina la Micky (16).

"Mama aliyejeruhiwa kwa kupigwa anaitwa Lusajo Mwasonge(40), ni mjasiriamali, alipigwa na kitu butu kichwani, anaendelea kupatiwa matibabu. Jeshi la polisi linatoa wito kwa wananchi wa Dodoma kama ulivyo utamaduni wao kuendelea kushirikiana na jeshi hilo ili kuhamimisha waliotekeleza uhalifu huu wanakamatwa na kufikishwa mahakamani," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri alisema jana kuwa mtu mmoja anashikiliwa na polisi kwa ajili ya mahojiano kuhusu undani wa tukio hilo.

Baba wa familia hiyo, Mwalimu Mgema anayefanya kazi Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, alisema kuwa Jumamosi alikwenda Dodoma kwa ajili ya mahafali katika Shule ya Msingi Chihoni na siku hiyo hiyo alirejea Singida kutokana na majukumu aliyokuwa amepangiwa na siku ya Jumapili aliwasiliana kwa ujumbe mfupi na mkewe.

"Jioni niliwahi kulala kutokana na uchovu, mke wangu alinitafuta saa tatu usiku na isivyo bahati sikusikia simu, asubuhi nilipoamka nikapiga simu, lakini sikufanikiwa kumpata hadi saa nane mchana na si kawaida, nikapigiwa simu saa 10 jioni na jirani yangu Baba Kelvin.

"Akasema nyumbani kwangu hakueleweki, hajaona anayetoka nje. Nikamwuliza 'hakuna mtu yeyote?'. Akasema 'kuna mtoto ndani anaitika, tunamwambia afungue mlango, anasema anaogopa'," alisema.

Alisimuliwa kuwa baadaye alipokea simu ya jirani mwingine ambaye alimpa taarifa kuwa wamemwangalia dirishani na kuona binti wa kazi amelala chini na kuna damu, alilazimika kuanza safari kutokana na taarifa hiyo.

"Nikiwa njiani ninakuja, nikapigiwa tena kuwa polisi wameingia watu watatu wamefariki, nikauliza 'ni kina nani?' Sikupata majibu, nikaambiwa polisi wanaendelea na uchunguzi na nilipofika muda wa saa moja jioni nyumbani na kuomba nioneshwe waliofariki dunia, na kuuliza kuhusu mtoto wangu mdogo anayeitwa Caren, nikajibiwa ndiye aliyefungua mlango," alisema.

Mwalimu huyo alisema kuwa nyumbani kwake aliacha watu watano; mabinti watatu wakubwa na kati yao, mmoja amehitimu darasa la saba na binti mdogo ndiye aliyebaki hai.

"Inasikitisha sana, sijawahi kuwa na uhasama na mtu, tuna miezi sita tumehamia pale, sina mgogoro na mtu yeyote, ninalaani vikali sana, hatuwezi kwenda kwa mtindo huu, wameua watu ambao wangekuja kutusaidia, wamezima ndoto ya mwanangu, alitaka kuwa mhandisi," alisema.

Jiji la Dodoma limekuwa na matukio ya mauaji yanayodaiwa kufanywa na watu wasiojulikana. Mwanzoni mwa mwezi huu, kuliripotiwa tukio la mama na mwanawe kuuawa katika Kata ya Mkonze, jijini.

Julai mwaka huu mtoto wa miaka minne alikutwa amefariki duania eneo la Nyumba 300, huku mwili wake ukikutwa hauna baadhi ya viungo.

Vilevile, wasichana wawili waliuawa kwa kupigwa na kuchomwa moto katika chumba walichokuwa wanaishi eneo la Nzuguni.

# UKUBWA WA DENI LA TAIFA

## -Kuna sababu Watanzania kutaharuki?

**Na Ludovick Utouh**

ILI kufikia Malengo ya Maendeleo Endelevu pamoja na malengo mengine ambayo nchi imejiwekea, ni lazima kufanyike uwekezaji mkubwa katika miradi ya kimkakati katika sekta mbalimbali kama nishati, afya, elimu, maji na kilimo na rasilimali watu.

Hata hivyo, serikali za nchi zinazoendelea zina changamoto/uwezo mdogo wa kukusanya mapato ya ndani yanayotosheleza kuendesha nchi. Hivyo basi, inazilazimu nchi/serikali kukopa na kuingia kwenye madeni ili kupata fedha za kutekeleza miradi ya kimkakati itakayochechemua uchumi na kuleta maendeleo. Hapo ndipo wananchi wanapoanza kusikia kuhusu Deni la Taifa au Deni la Serikali.

Deni la Taifa au Deni la Serikali ni deni ambalo lilikopwa na serikali kutoka katika vyanzo mbalimbali ndani na nje ya nchi na ambalo linapaswa kulipwa.

Madeni mara nyingi hutokana na hali ya mtu binafsi, familia au serikali kulazimika kukopa kwa sababu ya kuwa na bajeti ya matumizi ambayo ni kubwa kuliko mapato yanayotarajiwa kupatikana katika kufanikisha shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa kipindi husika.

Kwa lugha ya kihasibu, makisio/matarajio ya matumizi yanapozidi makisio/matarajio ya mapato, yanasababisha kuwapo nakisi/upungufu kwenye bajeti iliyotayarishwa.

Taasisi ya Kifedha (Corporate Finance Institute) inaeleza kuwa Deni la Taifa ni jumla ya madeni yote ambayo serikali au nchi inadaiwa. Mara nyingi madeni haya hutokana na hati fungani (bonds) pamoja na dhamana zingine za madeni, lakini pia Deni la Taifa hutokana na kukopa moja kwa moja kutoka katika taasisi za kifedha za kimataifa kama vile Benki ya Dunia (WB), Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) au nchi zilizoendelea.

Deni la Taifa ni njia mojawapo ya upatikanaji fedha za kujazia nakisi iliyojitokeza kwenye uandaaji bajeti ya taifa ya mwaka husika.

Utaratibu huu unatumika na unakubalika kwenye serikali zote duniani. Serikali zote duniani huwa zinajitahidi kuwa na uwiano wa mapato na matumizi katika kuandaa bajeti zao. Ili ziweze kutimiza azma hii, serikali nyingi zinalazimika kukopa kwa madhumuni ya kuleta uwiano wa mapato na matumizi ya kipindi husika.

Mikopo ya serikali nyingi inapatikana ama kutoka serikali nyingine au taasisi za fedha na benki. Benki zinazotoa mikopo zipo za aina mbalimbali, zikiwamo benki za biashara ambazo riba zake ni kubwa na masharti yake ya kukopa ni magumu zaidi ya benki nyingine.




CAG mstaafu Ludovick Utouh

**AINA YA MIKOPO**

Mikopo inayochukuliwa na serikali inaweza kuwa yenye masharti nafuu ya riba na dhamana au yenye masharti magumu ya riba na dhamana; pia inaweza kuwa ya muda mfupi au ya muda mrefu wa kulipwa.

Kwa kuwa mara nyingi mikopo ya aina hii ni ya kulipia gharama za miradi ya maendeleo (miradi ya kimkakati) ambayo huchukua muda mrefu kukamilika, inashauriwa aina ya mikopo inayochukuliwa kugharamia miradi hii iwe ya masharti nafuu ya riba (concessionary loans) na iwe ya muda mrefu wa kulipa (long term loans).

Vilevile, inashauriwa kuwa mikataba ya mikopo ya maendeleo iweke uwezekano wa kubadilisha masharti ya awali ya mikopo wakati wa utekelezaji miradi mikubwa ya maendeleo ili yaendane na uhalisia wa hali ilivyo kiuchumi, kisiasa na kiteknolojia.

Kutekelezwa kwa miradi ya kimkakati nchini husababisha ongezeko la ajira kwa wananchi; huongeza mzunguko wa fedha katika uchumi wa nchi; huimarisha miundombinu ya nchi na kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara; huboresha huduma zitolewazo kwa wananchi na huchochea kasi ya maendeleo ya nchi.

Mikopo ya aina hii mara nyingi hulenga katika kukuza uchumi wa nchi mara baada ya miradi ya kimkakati iliyolipiwa na fedha za mikopo hiyo kukamilika na kuanza kuzalisha bidhaa au huduma.

Deni la Taifa huhusisha madeni ya nje ya nchi na madeni ya ndani ya nchi. Nchi nyingi zinazoendelea hukopa nje aidha kwa mataifa rafiki wa nchi hizo au benki za nje zilizojizatiti kwenye kukopesha nchi zinazoendelea, zikiwamo WB, IMF, Benki ya Maendeleo ya Afrika na Benki ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mikopo ya ndani ya nchi mara nyingi hukopwa na serikali kutoka Benki Kuu ya nchi, mifuko ya hifadhi ya jamii na benki za biashara za ndani ya nchi.

Aina nyingine ya mikopo ya ndani ya serikali ni pale ambapo serikali inapopata huduma ambayo haijalipiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha wa serikali. Deni hilo linaweza kuwa ni la watumishi ambao hawajalipwa stahili zao ilipofika mwisho wa mwaka wa fedha wa serikali au madai ya makandarasi ambao wametoa huduma kwa serikali kwa makubaliano ya kulipwa lakini wanakuwa hawajalipwa mpaka mwaka wa serikali unapokuwa umeisha kutokana na serikali kutokuwa na fedha za kutosha kulipia madeni yake mwisho wa mwaka.

**UKUAJI WA DENI LA TAIFA**

Ukuaji wa Deni la Taifa unapaswa uendane na ukuaji wa uchumi wa nchi ili deni hilo liwe himilivu. Wakati Benjamin William Mkapa, Rais wa Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokuwa anamaliza muda wake mwishoni mwa mwaka 2005, Deni la Taifa lilikuwa Sh. trillioni 10.93 wakati uchumi wa taifa ukiwa na thamani ya Sh. trilioni 21.4 (Dola za Marekani bilioni 18.4).

Vivyo hivyo, wakati Rais wa Nne, Dk. Jakaya Kikwete alipokuwa anamaliza muda wake mwaka 2015, Deni la Taifa lilikuwa Sh. trilioni 41.82 wakati uchumi wa taifa ukiwa Sh. trlioni 84.28. Hii inaonesha kuwa, katika kipindi cha Dk. Kikwete, Deni la Taifa liliongezeka kwa asilimia 282.6 (zaidi ya mara mbili na nusu) kulinganisha na deni lililoachwa na Rais Mkapa.

Vilevile, Pato la Taifa lilikua kwa Sh. trilioni 62.88 sawa na asilimia 293.8 kutoka Sh. trlioni 21.44 hadi kufikia Sh. trilioni 84.28.

**INAENDELEA UK. 5**



Moja ya miradi inayotekelezwa kwa mikopo.

MAKALA MAALUM

INATOKA UK. 4

# UKUBWA WA DENI LA TAIFA

Katika kipindi cha Rais wa Tano, Dk. John Magufuli, Deni la Taifa liliongezeka hadi Sh. trilioni 72.3 kufikia mwezi Machi 2021 ikiwa ni ongezeko la Sh. 39 trilioni sawa na asilimia 72.8. Deni la Taifa lilikuwa ni asilimia 53.3 ya Pato la Taifa la Sh. trilioni 135.5 mwaka 2021.

Aidha, Deni la Taifa limefikia Sh. trilioni 111.3 mwezi Juni 2024. Ni ongezeko la Sh. trilioni 28.7 sawa na asilimia 54, ambapo uchumi wa taifa unatarajiwa kuwa wa thamani ya Sh. trilioni 230.91.

Ripoti ya Benki ya Dunia, "The World Bank Economic Report on Tanzania 2023", imetoa taarifa njema ya ukuaji uchumi wa nchi wa asilimia 5.2 kulinganishwa na ukuaji uchumi wa nchi mwaka 2022 wa asilimia 4.6.

Mbali na kuwapo ukuaji wa kuridhisha wa uchumi wa nchi, bado hali ya umaskini nchini haijapungua kwa kasi ya kuridhisha kutokana na kasi ya ongezeka la watu kwa kiwango cha asilimia tatu.

**UHIMILIVU WA DENI LA TAIFA**

Kabla mkopeshaji yeyote -- awe ni nchi, benki au mtu binafsi hajafanya uamuzi wa kukopesha fedha kwa mkopaji yeyote awe ni nchi, taasisi au mtu binafsi, ni lazima mkopeshaji awe na vigezo vya kumhakikishia kuwa mkopo atakaotolewa, utarejeshwa na mkopaji.

Vilevile, mkopaji naye anapaswa kuwa na uhakika wa kuwa na uwezo wa kurejesha mkopo anaotarajia kuuchukua kwa kuwa deni ni lazima lirejeshwe na mkopaji kwa aliyemkopesha.

Hivyo, nchi inapotaka kukopa huwa inafanyiwa tathmini ya uwezo wake wa kulipa mkopo unaoombwa ili mkopeshaji ajiridhishe kuhusu uwezo wa mkopaji kurejesha deni lililochukuliwa.

Vivyo hivyo, mkopaji naye anapaswa kujifanyia tathmini ya uwezo wake wa kulibeba deni analotarajia kulikopa na kujihakikishia kuwa ataweza kuwa na uwezo wa kulilipa deni hilo mara litakapoiva.

Kwa mfano, kwenye hotuba ya bajeti ya mwaka 2024/25, Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (Mb), alisema kuwa kwa mujibu wa tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2023, Deni la Taifa bado ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

"Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kuwa kwa mwaka 2023/24; uwiano wa Deni la Serikali kwa Pato la Taifa ni asilimia 35.6 kulinganisha na ukomo wa asilimia 55; uwiano wa deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 19 kulinganisha na ukomo wa asilimia 40; na uwiano wa deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 113.2 kulinganisha na ukomo wa asilimia 180," alisema Dk. Mwigulu.

Waziri huyo aliongeza kuwa hadi kufikia mwezi Machi 2024, Deni la Taifa lilikuwa Sh. trilioni 91.7. Kati ya kiasi hicho, deni la nje lilikuwa Sh. trilioni 60.95 na deni la ndani lilikuwa Sh. trilioni 30.75. Deni hili lilikuwa limeongezeka kwa Sh. trilioni 19.4 sawa na asilimia 26.8 ya deni lililoachwa na Rais wa Tano.




Mradi mwingine unaotekelezwa kwa mkopo.

**VIGEZO KUTATHMINI DENI LA TAIFA**

Benki ya Dunia (WB) hutumia Mfumo wa Uhimilivu wa Madeni (Debt Sustainability Factors - DSF) kufanya tathmini ya hatari za uhimilivu wa deni katika nchi zinazoendelea (Developing Countries). Vigezo vinavyotumiwa na WB katika kutathmini uhimilivu wa Deni la Taifa ni pamoja na:

Kwanza; Uainishaji Uwezo wa Kubeba Deni (Debt-Carrying Capacity Classification) - Nchi zinaanishwa kulingana na uwezo wao wa kubeba madeni uliotathminiwa ambao husaidia kubainisha uwezo wa nchi wa kusimamia na kulipa madeni yao kwa ufanisi.

Pili; Viashiria vya Viwango vya Mzigo wa Deni (Threshold Levels for Debt Burden Indicators) - WB huweka viashiria vya viwango vya juu vilivyochaguliwa vya upimaji wa mzigo wa deni kwa nchi husika kama vile uwiano wa Deni la Taifa kwa Pato la Taifa ili kujihakikishia uwezo wa nchi zinazokopa kuwa na uwezo wa kiuchumi kulipa madeni husika.

Tatu; makadirio ya msingi na matukio ya Jaribio la Mfadhaiko (Baseline Projections and Stress Test Scernarios) - Kigezo hiki kinapima namna gani nchi itaweza kustahimili mishtuko ya kiuchumi ya nje na ndani katika kulisimamia deni la nchi vizuri na kuweza kulilipa deni hilo mara litakapoiva.

Nne: Ukadiriaji vihatarishi vya dhiki ya deni (Risk Ratings of Debt Distress) - kwa kuchanganya kanuni elekezi na uamuzi wa wafanyakazi. Benki ya Dunia inazipanga nchi kulingana na viwango vya vihatarishi vinavyoweza kuathiri usimamizi mzuri wa ulipaji madeni ya taifa.

Tano: Ishara za Vihatarishi vya Kiufundi (Mechanical Risk Signals) - Kielezo cha DSF huzalisha mawimbi ya vihatarishi vya kiufundi kulingana na ulinganisho wa viashiria vya deni vya chini ya hali ya msingi na mkazo na vizingiti vinavyohusika kusaidia katika kubainisha viwango vya hatari vya dhiki ya deni la nje na la jumla la taifa.

Sita; Uchambuzi wa Mwaka wa Uhimilivu wa Deni (Annual Debt Sustainability Analysis (DSA)) - Benki ya Dunia huhitaji kila nchi mdeni wake kufanya uchambuzi wa uhimilivu wa madeni ya nchi zinazoendelea kila mwaka ukionesha hali halisi ya uhimilivu wa madeni ya nchi. Takwa hili la Benki ya Dunia huzipa nchi zilizokopa fursa ya kujifanyia tathmini zenyewe ili kujiridhisha kuhusu uwezo wao wa kuhudumia madeni waliyonayo na kujitathmini kama wana uwezo wa kuendelea kukopa.

Saba; Mwongozo wa Uamuzi wa Ukopaji na Ukopeshaji (Guidance for Borrowing and Lending Decisions) - Benki ya Dunia ina miongozo inayoongoza mkopeshaji kumfanyia mkopaji tathmini ya uwezo wake wa kukopa na miongozo inayomwongoza mkopaji kujifanyia tathmini ya uwezo wa kubeba na kulilipa deni analofikiria kukopa.

**NCHI BADO INA NAFASI KUKOPA**

Kwa kutumia vigezo vya kupima uhimilivu wa Deni la Taifa, Deni la Taifa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bado ni himilivu kama alivyotamka Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka 2024/25.

Deni hili ni himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu, hivyo serikali ipo kwenye hali nzuri ya kuendelea kukopa endapo kutatokea ulazima wa nchi kukopa.

Watanzania hatuna sababu ya kuogopa kukopa kwa ajili ya kuboresha miundombinu na huduma kwa wananchi na kuchochea kasi ya maendeleo ya nchi yetu.

**JUKUMU LA WANANCHI**

Kwa kuwa wananchi ndio wamiliki wa uchumi wa nchi kulingana na matakwa ya Katiba ya nchi ya mwaka 1977 (kama ilivyorekebishwa mara kwa mara) Ibara ya 8(1)(a) inayosomeka, "Wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii", ni lazima wananchi wawe na wajibu wa kuhakikisha mikopo inayochukuliwa na serikali itatumika kwa maendeleo ya nchi.

Wananchi wana haki ya kujua madhumuni ya mikopo inayochukuliwa na serikali na wana haki ya kijihakikishia kuwa mikopo inayochukuliwa na serikali inatumika kwa madhumuni yaliyokusudiwa na si vinginevyo.

Watanzania wengi walipongeza serikali chini ya uongozi wa Dk. Samia Suluhu Hassan kwa uwazi na uwajibikaji wa hali ya juu ulioonesha kwenye mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 wa Sh. trilioni 1.3 uliochukuliwa na serikali kwa shughuli mbalimbali za maendeleo nchini.

Uwazi na uwajibikaji wa aina hii ni mzuri na ni dalili za uimarikaji uwajibikaji na utawala bora nchini ambao unasisitizwa uendelezwe kwenye mikopo ijayo.

Ili kuimarisha uwajibikaji katika ukopaji wa serikali na kuongeza uwazi katika usimamizi wa Deni la Taifa, WAJIBU (taasisi anayoongoza hivi sasa) inashauri serikali kuweka wazi kwa wananchi nia yake ya kukopa, vyanzo vya mikopo, masharti ya mikopo pamoja na matumizi ya fedha za mikopo ili wananchi waweze kutambua mchango wa Deni la Taifa katika maendeleo ya taifa.

Hili linaweza kufanyika kwa kufanya mapitio ya Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134.

***Mwandishi wa uchambuzi huu ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) mstaafu. Hivi sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU.**

MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka kwa serikali kusikia kilio kuundwa tume huru

**KWA** miezi kadhaa kumekuwapo na taarifa za kutekwa kwa watu na wengine kukutwa wameuawa huku miili yao ikiwa na majeraha kuonesha kwamba kabla ya kufikwa na mauti, walipigwa na kuteswa na watekaji hao.

Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimekuwa kikilalamika mara kwa mara kwamba kimeathirika kwa kiasi kikubwa na matukio hayo kwa madai kuwa baadhi ya wanachama na viongozi wake wametekwa na hawajulikani waliko.

Pamoja na kulalamika huko, chama hicho kimekuwa kikiomba viongozi na wanachama hao waliotekwa wapatikane ama wakiwa hai au wamekufa. Sambamba na hilo kimekuwa kikilituhumu Jeshi la Polisi kuwa ndilo linalohusika kwa matukio hayo, huku lenyewe likisema hizo ni propaganda na chama kinaficha ukweli.

Hali hiyo ya utekaji ambayo pia imekuwa ikihusisha watu mbalimbali, ilipata uzito zaidi baada ya kuwapo kwa taarifa za kutekwa na watu waliodaiwa kuwa na silaha kwa aliyekuwa kada na Mjumbe wa Sekretarieti ya CHADEMA, Ali Kibao. Kada huyo alitekwa Dar es Salaam akiwa kwenye basi akienda Tanga na mwili wake kukutwa eneo la Ununio ukiwa umeharibiwa vibaya kiasi cha kushindwa kutambulika.

Kutokana na kifo hicho na kukithiri kwa matukio ya utekaji na mauaji ya watu, Rais Samia Suluhu Hassan alitoa maagizo kwamba uchunguzi wa kina ufanyike na apatiwe taarifa. Kauli hiyo iliungwa mkono na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Katibu Mkuu wake, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, ambaye alisema uchunguzi ufanyike kama ilivyoagizwa.

Wakati maagizo hayo yakitolewa na kuungwa mkono, kumejitokeza hoja kinzani kwamba Jeshi la Polisi wala vyombo vya ulinzi na usalama visifanye kazi hiyo kwa sababu baadhi vinatuhumiwa kushiriki matendo hayo ambayo yanatoa taswira hasi kwa Tanzania ambayo imejipambanua kwamba ni kisiwa cha amani na watu wake wanaishi kwa umoja na mshikamano. CHADEMA na makundi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini, wameshauri iundwe tume huru au tume ya kijaji kuchunguza suala hilo.

Juzi, wakati wa sherehe za Maulid zilizofanyika kitaifa mkoani Geita, Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) lilihanikiza jambo hilo kwamba ni vyema ikaundwa tume huru kuchunguza matukio hayo ya utekaji na mauaji ambayo yamekuwa yakifanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

Wazo la kuundwa kwa tume huru au ya kijaji ni mwafaka katika mazingira yaliyopo ili kuwapo kwa imani ya watu wote. Kama wahenga wasemavyo mganga hajigangi au kinyozi hajinyoi, ndivyo ilivyo kwa mazingira ya polisi kuchunguza jambo wakati wanatuhumiwa kuwa sehemu ya wahusika. Kwa ujumla, hakutakuwa na imani thabiti kama polisi watashiriki kuchunguza jambo hilo kwa sababu ni watuhumiwa.

Si mara ya kwanza kuundwa kwa tume huru au za kijaji kwa ajili ya kuchunguza jambo fulani lililojitokeza katika kwa kuwa ni utaratibu wa kawaida ili kuwafanya wananchi kuwa na imani na matokeo ya uchunguzi husika.


Waliomteka Kibao wanadaiwa kuwa askari waliokuwa na silaha na pia waliodaiwa kuwateka viongozi na wanachama wa CHADEMA walijitambulisha kuwa askari polisi, iweje sasa polisi hao hao ndio wahusike na uchunguzi? Tangu lini kesi ya nyani hakimu akawa nyani? Ni dhahiri kwamba kwa hali hiyo haki katu haiwezi kutendeka.

Kama viongozi wa vyama vya upinzani na BAKWATA walivyoshauri, ni vyema tume huru au ya kijaji hiyo ikaundwa ili ukweli ujulikane badala ya kufanyiwa na vyombo ambavyo vinadaiwa kuhusika na matukio yanayolalamikiwa.

Ni dhahiri kwamba kilio cha watu mbalimbali kimesikika na serikali ambayo imekuwa ikisema kuwa ni sikivu itakuwa imelipokea wazo hilo, kama Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alivyosema kuwa wanalifanyika kazi, ni imani kwamba jambo hilo litatekelezwa na hatimaye haki kutendeka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# ACT Wazalendo wameanza, vyama vingine vifuate

**MWENYEKITI** mstaafu wa Chama cha ACT Wazalendo, Juma Duni Haji, amezawadiwa gari ya kutembelea na chama chake, ikiwa ni utekelezaji wa sera ya kuenziwa viongozi wastaafu, kwa kutambua mchango wao kwa chama na taifa.

Kwa mujibu wa viongozi wa ACT Wazalendo, sera hiyo inakusudia kuwaenzi viongozi wastaafu ambao wakati wa uongozi wao, walikitumikia chama kwa heshima, bidii , uaminifu na uadilifu mkubwa.

ACT Wazalendo inawataja viongozi wanaohusika katika sera ya kuenziwa kuwa ni kiongozi wa chama na mwenyekiti wa chama wastaafu. Aidha, chama kinasema, wanapata posho ya kila mwezi pamoja na huduma hiyo wanapatiwa bima ya afya ambayo aina yake na posho ya kujikimu vitaamuliwa na Kamati ya Uongozi Taifa.

Kadhalika, wana sharti kuwa viongozi hao wasiwe wamekihama au kufukuzwa chama, wakitumikie chama kwa heshima na utii, huku Kamati ya Uongozi Taifa ikiwa na jukumu la kuamua iwapo kiongozi husika alikitumikia chama kwa heshima na utii.

Katika sera hiyo, chama kinasema, iwapo kiongozi atakuwa hana nyumba, chama kitamlipia pango la nyumba kwa kiwango ambacho kitaamuliwa na kamati hiyo , lakini pia kuna sharti kuwa viongozi hao wasiwe wamekihama au kufukuzwa chama, tena wawe wamekitumikia chama kwa heshima na utii, huku Kamati ya Uongozi Taifa ikiwa na dhamana ya kuamua iwapo kiongozi alitimiza takwa hilo.

Kwa utaratibu huo ACT Wazalendo, inastahili kuigwa na vyama vingine vya siasa, kutambua mchango wa viongozi wastaafu wa vyama vyao kwa kuwapa zawadi kama kumbukumbu ya huduma yao kwao na umma pia.

Huo ndio utaratibu wa sera ya chama hicho, ambao ninaamini unaweza kupunguza mtindo wa baadhi ya viongozi kuhama vyama vyao, badala yake watulie sehemu ili hatimaye wastaafu na kuenziwa.

Kwa kuwa lengo la kuwaenzi viongozi wastaafu ni kulinda heshima yao, kutambua mchango wao, kuendelea kunufaika na mawazo na fikra zao, katika ujenzi wa chama na kuwatunza na kuwahudumia kadri ya uwezo wa chama, utaratibu huo unafaa kuigwa hasa suala la afya.

Labda nami ningeongezea kidogo kwamba pamoja na huduma ambazo chama hicho kimeorodhesha kwa ajili ya wastaafu wake, hili la huduma ya afya kwa wastaafu wake limenigusa.

Ninaeleza hivyo, kwa sababu, moja ya vikwazo ambavyo wastaafu wengi wamekuwa wakikumbana navyo ni kukosa matibabu ya uhakika. Hicho ndicho kilio chao cha muda mrefu cha wazee na wastaafu.

Katika huduma ambazo chama hicho kimezibainisha, kwa ajili ya wastaafu wake, tiba au bima ya matibabu inaweza kuwa namba moja, hivyo kwa sera hiyo, vyama vingine vimepata cha kujifunza.

Ninadhani chama hicho kimetambua kuwa bila afya bora, hata hayo mengine ambayo kimepanga kuwafanyia wastaafu wake, hayawezi kuwa na maana bila kuwa na afya imara.

Huduma ya afya ni ya msingi kuliko huduma nyingine. Iwapo vyama vingine vitaamua kuiga baadhi ya vitu kutoka kwenye sera hiyo, basi vichukue hiyo huduma ya afya.

Iwapo hilo litafanyika, linaweza kuwafanya wanasiasa kuwa na uhakika wa kuhudumiwa afya zao hata wakiwa nje ya ulingo wa siasa, kuliko kuwaacha tu huku wakiwa na mchango kwenye vyama.

Ikumbukwe kuwa utumishi wa watu ni jukumu lisilolipika kwa gharama yoyote kwa vile wapo viongozi wanaotoa maisha na mali zao kwa ajili ya uhai wa taasisi kama vyama vya siasa. Mambo hayaishii hapo kuwatetea Watanzania wanyonge na kuibua shida zao ni jingine ambalo viongozi wa kisiasa wanalifanya. Ni jambo jema kuwathamani na kuwaenzi wafia siasa na maendeleo ya demokrasi ikibidi waanzishiwe makumbusho ya wanasiasa na watetezi wa siasa za kukosoa na kushauri serikali.

HABARI KITAIFA

# TASAC: Boti iliyozama ilikodishwa kubeba abiria

Na Elizabeth Zaya

SHIRIKA la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC), limesema boti ya wavuvi ndani ya Ziwa Victoria inayojulikana kama MV. MARWA KISS iliyozama Septemba 15, mwaka huu katika ziwa hilo ilikuwa imekodishwa kwa ajili ya kubeba abiria wanaokadiriwa kuwa 21.

Kwa mujibu wa TASAC, boti hiyo iliyokuwa ikitokea katika mwalo wa Iramba kuelekea mwalo wa Igundu wilayani Bunda mkoani Mara, mpaka juzi usiku abiria saba kati ya 21 waliodaiwa kuwapo kwenye boti hiyo walikuwa hawajapatikana na mwili mmoja jinsia ya kike ulipatikana.

Taarifa hiyo inaeleza kwamba, chanzo cha ajali hiyo ni boti kubeba na kuzidisha abiria kinyume cha sheria na kusababisha chombo hicho kutoboka na kuanza kuingiza maji.

Taarifa ya TASAC, ilifafanua kuwa abiria 14 waliokolewa na kati ya hao, 10 walikuwa ni wanaume na wanne ni wanawake na boti hiyo iliondoka saa moja usiku na kuzama saa 2.30 za usiku.

"Kazi ya utafutaji na uokozi wa miili hiyo bado inaendelea, abiria ambao hawajapatikana ni wanaume watano na wanawake wawili ambao majina yao hayakajulikana," ilieleza taarifa hiyo.

"Tumepokea kwa masikitiko taarifa ya kuzama kwa boti hiyo ambayo kwa kuwa hakikuwa ni chombo cha abiria, hapakuwa na vifaa okozi ndani hali iliyosababisha abiria kuzama ziwani.

Wakala huo ulikumbusha umma na wamiliki na wanaoendesha vyombo vidogo, kuhakikisha wanatumia vyombo vilivyosajiliwa kubeba abiria.

"TASAC inaendelea kusisitiza umma juu ya uzingatiaji wa tangazo namba 274 la mwaka 2024 likiwa na maelezo ya usalama kwa wamiliki wa vyombo vidogo, waendesha vyombo vidogo na abiria ikiwamo wananchi kuhakikisha wanatumia vyombo vilivyosajiliwa kubeba abiria.

"Kuwa na vifaa vya uokozi ndani ya chombo, kujiepusha kusafiri usiku na vyombo vidogo na wamiliki wa vyombo vya uvuvi kujiepusha na tamaa ya kubeba abiria kinyume cha sheria na kuhatarisha maisha ya watu."

TASAC ilisema itachukua hatua za kisheria dhidi ya mmiliki wa chombo hicho cha usafiri kwa kukiuka tangazo hilo.



Mmoja wa wakazi wa Kata ya Nyatwali, wilayani Bunda, mkoa wa Mara (mwenye kilemba chekundu), akijiandikisha juzi, ili kulipwa fidia, katika zoezi linaloendelea la kuhamisha wakazi wa kata hiyo, kupisha eneo la ushoroba wa Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# ACT: Kata tatu hazijatambuliwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa

## -Waliouza ardhi ya wananchi kukatwa

Na Halfani Chusi

KIONGOZI wa Chama cha ACT Wazalendo, Dorothy Semu, amedai kata tatu za Ulyankuku (Tabora) pamoja na Katumba na Mishamo (Katavi) hazijatambuliwa katika Tangazo la Mipaka ya Vijiji12,333, vitongoji 64,274 na Mitaa 4,269 vitakavyohusishwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika Novemba mwaka huu.

Dorothy amesema kuwa mbali na maeneo hayo, chama hicho pia kitafanya uchambuzi wa haraka ili kubaini maeneo mengine yaliyoachwa na serikali katika mchakato huo.

Mkuu wa Kitengo cha Habari Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Nteghejwa Hosseah, alipoulizwa na Nipashe jana kuhusu kata hizo kutotambuliwa, alisema kuwa anafuatilia kujua ukweli wa madai hayo.

Akihutubia wananchi wilayani Lushoto, mkoani Tanga juzi ikiwa ni mwendelezo wa ziara za viongozi wakuu wa chama hicho waliojigawa kikanda, Dorothy alidai kata hizo hazijatambuliwa katika tangazo hilo la serikali.

Dorothy alisema, "Kwa harakaharaka tumeona kata za Ulyankulu, Katumba na Mishamo kutotambuliwa kwenye mchakato huu uliotangazwa, kata hizi zilipewa hadhi ya kuwa maeneo halali ya wananchi baada ya kutoka kuwa makazi ya ukimbizi.

"Kwa mara ya kwanza Watanzania wapya walishiriki uchaguzi wa serikali mwaka 2015 na 2020, lakini serikali imeendelea kuwanyima haki ya kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji," alidai Dorothy.

Alisema ACT Wazalendo ilikuwa na shauku ya kuona serikali kama itizingatia kilio cha Watanzania wa Ulyankulu, Katumba na Mashimo, lakini kwa tangazo lililotolewa na TAMISEMI, imeendelea kuwaacha na kilio.

"Niwahakikishie Watanzania timu yetu makini ya chama itafanya uchambuzi haraka kuona kama kuna vijiji, mitaa na vitongoji vingine vimeachwa kufuatia na tangazo hilo kisha tutautaarifu umma," alisema Dorothy.

Katika ziara hiyo, Dorothy pia alihimiza Watanzania na wananchi wa Mkoa wa Tanga kujitokeza kwa wingi Novemba 27, mwaka huu kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji ili kutumia haki yao ya kikatiba ya kuchagua na kuchaguliwa.

"Mjitokeze kupiga kura, msitishike na vitisho vya aina yoyote, nenda mkakichagueni ACT- Wazalendo, ndiyo chama mbadala kwa sasa kitakachowaletea maendeleo," alisema Dorothy.

Pia alikemea kitendo cha baadhi ya viongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kuwafanyisha kazi wazee ndipo wapewe fedha.

Akiwa jimboni Bumbuli, Dorothy alisema, "Ili mzee wa Bumbuli apate fedha lazima afanyishwe kazi, hiyo si sawa na huko tunakoelekea tutaaimbia Benki ya Dunia iache kutoa hizo fedha kwa kuwa zimegeuka mateso na si msaada kwa kaya maskini."

## KABWELA

Na Fadhili Mohammed



# Hospitali Sanitas yaamriwa kuilipa NSSF bil. 1.3/-

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ndogo Dar es Salaam, imeiamuru Hospitali ya Sanitas Limited kuupa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Sh. bilioni 1.3 ikiwa ni michango ya wanachama pamoja na malimbikizo ya adhabu kuanzia Agosti 2013 hadi Mei 2024.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi mbele ya Jaji Elizabeth Mkwizu baada ya kusikiliza hoja za mlalamikaji.

Mlalamkaji katika shauri hilo ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) na NSSF ambao mahakamani waliwakilishwa na Wakili Kennedy Kasongwa.

Katika hati ya madai Hospitali ya Sanitas inadaiwa Sh. 1,357,453,580.96, kiasi hicho cha fedha kinajumuisha michango ya Sh. 903,541,612.62 ya wanachama ambayo haijalipwa pamoja na malimbikizo ya adhabu kuanzia Agosti 2013 hadi Mei 2024, Sh. 453,911,968.34.

Inadaiwa mlalamikiwa ni mwanachama wa NSSF alitakiwa kwa mwezi kuchangia jumla ya asimilia 20, asilimia 10 kutoka kwa wafanyakazi na asimilia 10 kutoka kwa mwajiri, lakini alishindwa kupeleka michango hiyo.

Hospitali ya Sanitas ilifikishiwa wito wa mahakama kupitia tangazo gazetini, mlalamikiwa huyo alishindwa kufika na alishindwa pia kuwasilisha mahakamani utetezi wake ndani ya siku 21. "Ukosefu huu wa usikilizaji unazua wasiwasi mkubwa na inaonekana hakuna sababu ya msingi ya kuahirisha kesi kwa muda usiojulikana," alisema Jaji Mkwizu.

Alisema kutokana na mazingira hayo Mahakama inatoa hukumu kwa faida ya mlalamikaji.

"Mahakama inamwamuru mlalamikiwa kulipa jumla ya Sh. 1,357,453,580.96 ikiwa ni michango ya wafanyakazi pamoja na malimbikizo ya adhabu. "Mahakama inaamuru mlalamikiwa kulipa faida ya asilimia 15 kuanzia Mei, mwaka huu hadi tarehe ya hukumu Septemba mwaka huu, ameamuliwa kulipa asilimia saba kwa mwaka kuanzia tarehe ya hukumu hadi atakapomaliza kulipa fedha zote anazodaiwa na mwisho mlalamikiwa anatakiwa kulipa gharama za kesi," alisema Jaji Mkwizu.



Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Irene John, akizungumza wakati wa mafunzo ya usimamizi wa mazingira kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ukatili kwa watoto waongezeka asilimia 57

**Na Pilly Kigome**

ONGEZEKO la vitendo vya ukatili ikiwamo ubakaji na ulawiti kwa watoto vinatishia amani na kwa takwimu za msingi za mwaka 2023 zinaonesha matukio hayo kuongezeka kwa asilimia 57.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Shirika la WAJIKI, Janeth Mawinza, alipokuwa akizungumza katika matembezi maalum yaliyowakutanisha wadau wa watetezi wa haki za watoto kupinga vitendo vya ukatili yaliyofanyika mkoani Dar es Salaam.

Mawinza alisema vitendo vya ulawiti vimeongezeka kutoka kesi 1,205 mwaka 2020 hadi 2,488 mwaka 2023 na ubakaji vimeongezeka kwa kasi kutoka matukio 6,827 mwaka 2022 hadi 8,691 mwaka 2023.

Alisema kutokana na takwimu hiyo na vitendo hivyo kushamiri inadhihirisha jamii isiyo salama kwa watoto na kwamba juhudi za kina kwa serikali na wadau kupaza sauti kukemea vitendo hivyo zinahitajika.

Mkurugenzi wa TAWLA, Tike Mwambipile, alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuendelea kusisitiza ulinzi na usalama wa watoto nchini kukamilisha kwa haraka haki dhidi ya waathirika wa vitendo vya ukatili.

Mwambipile alimwomba Rais awawajibishe Waziri wa Mambo ya Ndani na IGP na kuunda vyanzo vya uchunguzi kwa kuwa hawaridhishwi na kasi ya ufuatiliaji inayochukuliwa na viongozi hao katika kesi zilizowakilishwa dhidi ya vitendo vya ukatili nchini.

Aidha, aliliomba Bunge kupitia upya kufanya mapitio ya sheria ya kanuni ya adhabu ili kufuta dhamana kwa makosa yote ya ubakaji na ulawiti kwa watoto kwa kuwa hiyo inaonekana ni chanzo cha ongezeko la vitendo hivyo.

"Tunaona mhalifu anakamatwa, lakini inasikitisha kuona mtuhumiwa huyo akiachiwa na kuwa nje jambo ambalo linasikitisha na kuwafanya wahanga na jamii kuishi kwa uoga kwa kurejea kwa wahalifu hao katika jamii," alisema.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), kwa kushirikiana na mashirika wanachama ambao ni watetezi wa haki za watoto wameungana katika matembezi ya amani ya kuhimiza ulinzi wa haki za watoto wa Tanzania kwa kaulimbiu "Hakuna ukimya tena tunadai ulinzi wa watoto wetu kwani Tanzania bila ukatili kwa watoto inawezekana".

Huu ikiwa ni mwendelezo wa harakati ambazo THRDC imekuwa ikizifanya kwa kusapoti wanachama wake kutetea haki za watoto nchini na hatua ya matembezi ya amani imechukuliwa na wanachama hao wa haki za watoto kama mojawapo ya njia ya kuonyesha hali mbaya ya ukatili wa watoto iliyoko katika jamii na kuonyesha kutoridhishwa na matukio hayo yanayoshamiri katika jamii yakiwamo ya mauaji, ulawiti, ubakaji, utekaji na hata utumikishwaji dhidi ya watoto.

"Tunalaani vikali vitendo vya kubakwa, kulawitiwa, kutekwa, kupotea, kuibiwa na mauaji ya watoto vinavyoripotiwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kwani vitendo hivi vinadidimiza hali ya usalama wa watoto nchini na pia ni kinyume na haki za binadamu," alisema.

# NEMC yataja sababu kuchelewa kupata TAM

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema uelewa mdogo wa wawekezaji kuhusu matakwa ya kisheria ndiyo umesababisha kuchelewa kupata cheti cha Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kwenye miradi yao.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Meneja wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii wa NEMC, Jamal Baruti, wakati akizungumzia mchakato wa kupata cheti hicho.

Alikuwa akizungumza kwenye mafunzo ya siku moja yaliyoandaliwa na NEMC kwa waandishi wa habari kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004.

Alisema uelewa mdogo wa matakwa ya kisheria kutoka kwa wawekezaji, wataalamu elekezi, wadau na jamii kwa ujumla kumekuwa kikwazo kwa mchakato huo kuchukua muda mrefu.

Alisema baadhi ya wawekezaji wanatoa malalamiko kwamba NEMC inachelewa kuwapa cheti hicho wakati wenyewe ndiyo wameshindwa kukidhi vigezo husika kwa wakati.

"Baadhi wanataka kupata EIA ili waweze kupata huduma zingine za serikali kama kibali cha uwekezaji kwa hiyo mtu anapata mkopo anakuja spidi NEMC anaanza kutoa msukumo apewe haraka na wakati mwingine hakidhi vigezo vinavyotakiwa," alisema.

Alisema baadhi ya wawekezaji huanzisha mchakato wa kupata cheti cha TAM katika hatua za mwisho za uwekezaji baada ya kupata mkopo na maeneo ya kwenda kuwekeza.

Alisema kuna wakati hadidu za rejea kwa ajili ya kupata cheti hicho hazikidhi viwango na taarifa za mradi husika na kulazimika kurudi kwa ajili ya kukamilisha vigezo husika.

Alisema baadhi ya wawekezaji wanaomba kupewa cheti cha TAM lakini maandiko yao ya miradi yanakosa takwimu za kitaalamu na wakati mwingine kuchelewesha wenyewe kuwasilisha maombi yao ofisi za NEMC.

Baruti alisema uwekezaji unapaswa kuzingatia mipango miji na matumizi bora ya ardhi na kuongeza kuwa kuna umuhimu wa kujengea uwezo taasisi ili kusimamia ipasavyo mazingira.

Alisema NEMC inaendelea kutoa elimu kwa jamii ya wafanyabiashara na wawekezaji kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira ili wasione kuwa kukidhi matakwa ya kisheria ya kupata cheti cha EIA ni usumbufu kwao.

Alisema NEMC inaendelea kusimamia sheria kuhakikisha miradi yote mikubwa na midogo inasajiliwa bila shuruti na mapema katika hatua za uwekezaji ili kuepuka usumbufu.

Meneja Mawasiliano wa (NEMC), Irene John, alisema Baraza litaendelea kuwapa mafunzo ya uhifadhi wa mazingira waandishi wa habari ili kuwajengea uwezo wa kuandika kwa usahihi masuala yanayohusu mazingira.



# Naibu Waziri apigia chapuo matumizi ya gesi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Mwanaidi Ali Khamisi, anasema nishati safi ya gesi ya kupikia majumbani ni rafiki wa mazingira na inavutia mamilioni ya watu ulimwenguni kuitumia.

Akizungumza jana katika kongamano la wanawake lililofanyika Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Mwanaidi, alisema serikali inafanya kila linalowezekana kushusha bei ya gesi ya kupikia, ili ipatikane kwa gharama nafuu kwenye maeneo yote nchini.

Wiki iliyopita, Wakala wa Nishati Vijijini (REA), iliingia mikataba sita ya utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Miongoni mwa mikataba hiyo, ni wa kusambaza mitungi 450,000 ya gesi ya kilo sita katika maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji, utakaotekelezwa na Kampuni za Manjis, Oryx, Lake Gas na Taifa Gas, ambapo serikali kupitia REA, itatoa ruzuku ya hadi asilimia 50 kwa wananchi ili kununua mitungi hiyo.

**"Serikali imeendelea kuongeza jitihada za kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, hasa kwa wanawake wa vijijini. Wilaya ya Same ni mojawapo, kwamba nia wanawake..."**

"Serikali imeendelea kuongeza jitihada za kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, hasa kwa wanawake wa vijijini. Wilaya ya Same ni mojawapo, kwamba nia wanawake waondokane na matumizi ya nishati chafu ambazo zina athari kiafya pamoja na kimazingira," alisema.

Kwa mujibu wa Meneja wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Kanda ya Kaskazini, Lorivii Long'idu, baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanahujumu nishati hiyo kwa kuchakachua ujazo wa mitungi ya gesi na kuuza ikiwa na ujazo pungufu.

Kuhusu suala la uagizaji, uhifadhi, usambazaji na ujazaji wa gesi ya kupikia majumbani, alisema ni lazima ijazwe kwa kuzingatia uzito ulio sahihi kama unavyoonyeshwa kwenye mitungi. Mkuu wa Wilaya ya Same, Kasilda Mgeni, alisema jitihada zinazofanywa na serikali mpaka sasa ni kuhamasisha wanawake kuondokana na matumizi ya nishati chafu ya kupikia.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Batilda Buriani (wa pili kulia), akipokea zawadi ya vazi la ubunifu lililonakshiwa kwa kanga za kale, lililobuniwa na Mbunifu wa Kimataifa, Pichichi Turbans (kulia), jijini Tanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA**

# DC awapa mbinu wadau wa alizeti kuwa mabilionea

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Wilaya ya Babati, mkoani Manyara, Emmanuela Kaganda, amewataka wakulima wa alizeti na wafanyabiashara ya mafuta ya kula, kujifunza na kujipanga kuhudumia masoko makubwa ya ndani, kikanda na kimataifa ili kutengeneza mabilionea wa zao hilo.

Alisema kufunguka kwa Soko la Eneo Huru la Afrika (AfCFTA), ambalo linakadiriwa kuwa na walaji zaidi ya bilioni 1.3 kutoka nchi 53 Afrika ni fursa kubwa kwa wafanyabiashara wa Tanzania.

Kaganda alikuwa akizungumza juzi na wakulima na wadau mbalimbali wa sekta ya kilimo, wakati wa hafla ya utiaji saini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa uendelezaji wa zao la alizeti.

Mkataba huo ulihusisha kati ya Taasisi ya Maendeleo ya Afrika ya US African Development Foundation (USADF) na Chama cha Ushirika wa Kilimo na Masoko cha Mbungwe.

"Ni muhimu sana tukaweka jitihada za dhati kuyafikia masoko haya na siyo kuwa waangaliaji tu na kulalamika. Niwaombe sana wataalamu wa serikali, kuwasimamia wakulima.

"Na katika mradi huu, niwahakikishie USADF, kwamba Mbugwe AMCOS itafanya vizuri na kupata Dola za Marekani 250,000. Kupitia mradi huu pia, matumaini ya serikali ni kuanzisha viwanda na kutengeneza mabilionea."

Mkoa wa Manyara ni kati ya mikoa nchini inayolima alizeti lakini tija ni ndogo kutokana na wakulima wengi kutumia mbegu za kienyeji ambazo hazijafanyiwa utafiti.

Watafiti na wahaulishaji wa teknolojia za kilimo kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), wamekuwa wakieleza katika machapisho mbalimbali nchini kuwa, hivi sasa mbegu ya 'record' na mbegu nyingine mpya zilizofanyiwa utafiti, ambazo zimetambulishwa kwa wakulima waanze kuzitumia, kwa kuwa zina tija kubwa.

TARI inahamasisha matumizi ya mbegu hizo, kwa sababu zinastahimili mabadiliko ya tabianchi na bei ya wastani ambayo wakulima wengi wanamudu kununua, lakini pia zina tija katika uzalishaji.

Katika hafla hiyo, Mrajis Msaidizi wa Vyama vya Ushirika mkoani Manyara, Absalum Cheliga, alisema mradi huo umekuja kuwanyanyua kiuchumi wana ushirika na unagusa uzalishaji na masoko.

Kwa upande wake, Ramadhan Mangi, alisema Mbugwe AMCOS, itaongeza thamani na wakulima, watapata fedha nyingi hivyo aliwashauri wafanye kazi kwa bidii na kulima kwa wakati na kupanda kwa wakati ili wapate mazao mengi.

# Wamiliki migodi wapewa siku 90 kuweka matangi ya maji

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

OFISA Madini Mkazi wa Mirerani, Nchagwa Marwa, ametoa siku 90 kwa wamiliki wa migodi ya madini ya tanzanite iliyoko katika Mji Mdogo wa Mirerani mkoani Manyara, kuhakikisha kila mgodi unakuwa na matangi ya maji, ili kuepuka maradhi ya vifua kwa wachimbaji.

Alisema hayo jana wakati akizungumza na wachimbaji wa madini ya tanzanite juu ya usalama migodini.

Pia aliwasisitiza kufanya uchimbaji salama kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za madini na kusema baada ya miezi miwili watafanya ukaguzi.

"Tunapaswa kuhakikisha kuwa kila mgodi unakuwa na tangi la maji lenye ujazo wa kuanzia lita 1,000 yatumike mgodini hasa wakati wa kuchoronga miamba ili kuondoka vumbi linalosababisha maradhi," alisema Nchagwa.

Hata hivyo alisema ni vyema wachimbaji madini wakachukua tahadhari kwa kuhakikisha wanatumia maji kuepusha maradhi yanayosababishwa na vumbi mgodini.

"Nategemea baada ya miezi miwili matangi yawepo na kila mgodi ufunge simu kutoka mgodini hadi juu ili kurahisisha mawasiliano pindi kukitokea tatizo," alisema Nchagwa.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha (AUWSA), John Ndetiko, alisema wamejipanga kuhakikisha wanafikisha maji ndani ya ukuta wa madini ya tanzanite na kuuza kwa bei nafuu.

Aidha, Ndetiko, alisema wanatarajia kuuza maji lita 1,000 kwa Sh. 3,000 wakati wakifanya mikakati ya muda mrefu kufikisha maji ya bomba kwenye migodi ya madini ya tanzanite.

Akizungumza na wadau hao wa madini, Dk. Alexander Mbuye, anayejihusisha na udhibiti wa magonjwa ya kifua kikuu, maambukizi ya VVU, alisema maji ni muhimu kwenye uchimbaji.

"Njia pekee ya kuzuia kuvuta vumbi kuepuka silicosis migodini ni kutumia maji mengi kwa kuwa ugonjwa hauna dawa baada ya mapafu kuathirika na vumbi," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Manyara (MAREMA), Tawi la Mirerani, Peter Laizer, alisema suala la wachimbaji kuwa na tangi la maji lita 1,000 halina mjadala kwani ni kwa ajili ya manufaa ya wachimbaji madini.

"Kama nyumbani mtu na familia yake anakuwa na tangi la lita 3,000 kwenye machimbo ya madini ya tanzanite pia inatakiwa awe na tangi la 1,000 ili kufanikisha uchimbaji salama," alisema.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alisema wachimbaji wanapaswa kutekeleza suala la maji na kuweka simu kwa ajili ya mawasiliano mgodini.

Mchimbaji wa madini, Zephania Joseph, alisema anaunga mkono kuwapo na matangi ya maji kwa wachimbaji kwa ajili ya kuondoa vumbi mgodini baada ya kulipuliwa na baruti.





# Wazee wataka uwakilishi bungeni kupenyeza kero zao

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

BARAZA la Ushauri la Wazee mkoani Shinyanga, limeomba ushirikishwaji wa wazee katika vikao vya maamuzi kuanzia ngazi za chini pamoja na uwakilishi kwenye mabaraza ya madiwani na bungeni.

Limesema lengo ni kufikisha moja kwa moja mahitaji yao yafanyiwe utekelezaji wa haraka.

Hayo yalibainishwa juzi na Ofisa Ufuatiliaji masuala ya wazee, Laurent Mihayo, wakati akiwasilisha mahitaji na mapendekezo ya wazee wa Halmashauri ya Ushetu kwa Katibu wa Mbunge wa Ushetu, Elizabeth John kwa niaba ya Mbunge Emmanuel Cherehani.

Alisema wazee kukosa uwakilishi kwenye vikao vya maamuzi ikiwamo bungeni, mambo yao mengi yamekuwa yakikwama kutekelezwa, likiwamo suala la utungwaji wa sheria ya wazee, ambapo wamekuwa wakiahidiwa itatungwa.

Alisema endapo wazee wangekuwa na uwakilishi bungeni suala la kilio cha kutungiwa sheria inayowahusu lingekuwa historia, lakini sasa hivi wanapiga kelele kila kukicha lakini hakuna utekelezaji.

Kadhalika alieleza uhitaji wa sheria ya kuwabana watoto ili kuwatunza wazee na siyo kuwatelekeza kama ilivyo sasa kwa wazee wengi na kubaki kuwa omba omba.

Mapendekezo mengine ni wazee wanaume wanaomba na wao wakumbukwe kwenye mikopo ya halmashauri ya asilimia 10, sababu wapo ambao wana nguvu na wanaweza kufanya shughuli za kiuchumi na kujikwamua kimaisha.

Mjumbe wa Baraza la Wazee Halmashauri ya Ushetu, Majaliwa Lukuba, aliisisitiza serikali iendelee kuboresha huduma bila malipo kwa wazee, pamoja na kuwapatia vitambulisho vya matibabu bure, kwamba kuna baadhi ya wazee hawana vitambulisho hivyo.

Katibu wa Mbunge wa Ushetu, Elizabeth John, alisema mahitaji na mapendekezo ya wazee hao ni ya msingi na kwamba baadhi Mbunge Cherehani alishaanza kuyasemea bungeni.

Aliyataja yaliyotekelezwa ni suala la mikopo asilimia 10 ya halmashauri kwa watu wenye umri wa kuanzia miaka 36 na kuendelea, huku akiahidi mapendekezo yao atayafikisha kwa mbunge.

# Madiwani wa Igunga watoa maagizo makandarasi wavivu

**Na Halima Ikunji,** IGUNGA

BARAZA la Madiwani katika Halmashauri ya Wilaya ya Igunga Mkoani Tabora limeutaka Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), kutokuwapa kazi makandarasi wanaochelewesha miradi kwani wamekuwa wakisababisha mkwamo wa shughuli za kimaendeleo.

Madiwani hao akiwamo Robert Jidai wa Kata ya Nanga, wametoa malalamiko hayo kwa nyakati tofauti katika kikao cha baraza la madiwani cha robo ya nne na kuitaka TARURA kuwa na usimamizi makini katika miradi hiyo ya umma.

Jidai alisema kuna mkandarasi aliyepewa kujenga barabara ya kutoka Nanga, Mwabaraturu hadi Itunduru tangu Aprili, 2024 bado hajafika eneo la kazi, huku wananchi wakiendelea kupata shida ya ukosefu wa barabara.

Alidai kinachosikitisha mkandarasi huyo hana vifaa vya kufanyia kazi, hivyo aliitaka TARURA isiwe inatoa kazi kwa makandarasi kama hao, kwamba wanakwamisha juhudi za serikali na kusababisha wananchi kuichukia.

Diwani wa Kata ya Itumba, Jilala Mipawa alisema Barabara ya Igunga hadi Itumba ina mashimo marefu hali ambayo imekuwa ikisababisha magari kupata ajali mara kwa mara, huku akishangazwa na TARURA kutofukia mashimo hayo wakati fedha za dharura zipo.

Diwani wa Kata ya Mwashiku, Mishamo Lubyalo, alisema kwenye kata yake kuna daraja kubwa la Kadoto ambalo lilibomolewa na mvua baadhi ya maeneo, hivyo juhudi za kulirudisha zinahitajika haraka ili kuwanusuru wananchi wasipate shida nyakati za masika.

> **"Mawakala hao watasaidia kutambua waombaji wa eneo husika na hivyo kupunguza kutokea kwa vurugu zisizokuwa za lazima, lakini hawaruhusiwi kuwaingilia watendaji ...**

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Lucas Bugota, alimtaka Meneja wa TARURA kuyafanyia kazi kwa haraka maeneo yote ya barabara yaliyolalamikiwa na madiwani katika kata zao ikiwa ni pamoja na kuwafuatilia kwa karibu makandarasi wote waliopewa kazi ili wamalize kwa muda waliopewa.

Akijibu malalamiko ya madiwani hao, Kaimu Meneja wa TARURA Wilaya ya Igunga, Adam Nalimi, alikiri mkandarasi aliyepewa kujenga Barabara ya Nanga-Mwabaraturu hadi Itunduru (km 14.93) na daraja moja lenye urefu wa mita 30 kwa thamani ya Sh. milioni 475.

Alisema kampuni inayojenga ni ya TINTON CO. LTD ya jijini Dar es Salaam ambapo mkataba alisaini Mei, 2024 na anatakiwa kukamilisha ujenzi Februari, 2025.

Hata hivyo aliwaomba madiwani kuwa wavumilivu kwa kuwa tayari walishamfuatilia na wakati wowote atafika eneo lake la kazi kuanza kazi.

Aidha, alikiri pia kuwapo kwa mashimo marefu katika barabara ya kutoka Kata ya Igunga hadi Kata ya Itumba na kusema kuwa tayari Sh. milioni 230 za dharura zimetengwa na kuahidi kutengeneza maeneo yote korofi ikiwamo Barabara ya Itumba.

Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Sauda Mtondoo aliwaomba madiwani kwenda kusimamia miradi yote inayopelekwa na serikali katika maeneo yao ikiwa pamoja na kuhakikisha inajengwa kwa kiwango.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Mboni Mhita (kulia), akizungumza na wafanyabiashara katika kikao kazi kilichoitishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Yusuph Mwenda, wilayani humo jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Wakulima watakiwa kuweka 'Made in Tanzania' katika mazao

**Na Judith Julius,** NGARA

NAIBU Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, amewataka wakulima wa mazao mbalimbali katika maeneo ya mpaka wa Rusumo wilayani Ngara, kuhakikisha wanaweka lebo za 'Made in Tanzania' kwenye vifungashio vya mazao yao, ili kuongeza thamani ya bidhaa hizo kimataifa.

Alitoa kauli hiyo juzi alipotembelea na kukagua shughuli katika Kituo cha Forodha kilichoko katika mpaka huo unaotenganisha nchi za ya Tanzania na Rwanda.

Kadhalika Kigahe alisikitishwa na taarifa za watu kutoka nchi jirani kuingia mashambani na kulangua mazao kwa wakulima kinyume na utaratibu hali inayorudisha nyuma bidhaa za ndani.

Pia, aliwataka wafanyabiashara hao kutoka nje kuacha mara moja na kuwataka watumie utaratibu maalum likiwamo Soko la Kimkakati la Kahaza ambalo linajengwa ili lisaidie wakulima kukusanya mazao kutoka shambani.

Meneja wa Kituo cha Forodha cha Rusumo, Amos Illoyo, alisema kituoni hapo wanakusanya mapato ya serikali na kudhibiti biashara za magendo zinazofanywa maeneo yanayozunguka mpaka ili kuwezesha ulipaji kodi na kuzuia bidhaa bandia.

Aidha, mpaka wa Rusumo umekuwa ni lango kuu la kupitisha bidhaa kwenda nchi za Rwanda na DR Congo, huku bidhaa zinazosafirishwa kwa wingi zikiwa ni saruji na vinywaji baridi.

Ofisa Biashara wa Wilaya ya Ngara, Privanus Katinhila, aliahidi kutekeleza maelekezo yaliyotolewa na waziri huyo kwa wakati, ili biashara mpakani hapo ziwanufaishe Watanzania.

Ukurasa 14





**NDIVYO WAGOMBEA URAIS MAREKANI WALIVYOCHUANA**

Ukurasa 12



**Wasomi wanavyomuunga mkono Rais wakihubiri nishati safi, ulinzi hifadhi**


# siasa

JUMATANO SEPTEMBA 18, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


MAUAJI NA UKATILI UNAOENDELEA...

# Imetimu wakati wa kuanza kutumia Mahakama ya Korona

## • Iko kisheria, japo wengi hawaifahamu

**Na Aidan Mbuguye**

KUNA matukio ya madhara vikiwamo vifo vyenye utata vinavyosikika nchini, vinavyoacha maswali, hofu pia kuanzisha mjadala mkubwa unaoendana na mapendekezo ya nini kifanyike.

Mbali na wanajamii, hata wanasiasa na viongozi wa dini kukemea, sasa imevuka mpaka kimataifa, wiki iliyopita mabalozi wa nchi 15 nao wanaeleza kushtushwa na hali hiyo.

Wakati hayo yakitokea kipo chombo rasmi kisheria cha kushughulikia hali hiyo na kuelekeza hatua zaidi za kufuata yanapotokea matukio ya hovyo kama hayo.

Ni Mahakama ya Korona, ambayo ni chombo huru chenye mamlaka ya kuchunguza sababu na mazingira ya kifo au vifo vinavyotokea katika mazingira tata.

Lengo la mahakama hiyo ni kubaini sababu na mazingira ya kifo na kutoa mapendekezo, ili kuepuka vifo vya aina hiyo visijirudie.

Mahakama hiyo huundwa kwenye wilaya kifo kinapotokea, kutokana na amri inayotangazwa kwenye gazeti la serikali na waziri mwenye dhamana, baada ya kumshirikisha Jaji Kiongozi.

Inatajwa kuwa mahakama hiyo iko kisheria kuchunguza vifo kwa mujibu wa sura ya 24 ya sheria ya Mahakama ya Korona. Kimuundo, inajumuisha mahakimu wa wilaya, watumishi wa umma waliopo kazini au waliostaafu na kila anayeunda mahakama hiyo, atatambulika kwa jina Korona.




Mahakama Kuu ya Korona nchini Marekani, mfano wa huduma inayohitajika ianzishwe nchini. **PICHA: MTANDAO**

Kazi za Mahakama ya Korona ni kuchunguza kifo cha aliyeuwawa kikatili au kisicho cha kawaida. Pili kama ni kifo cha ghafla na kuwezesha sababu zake zijulikane.

Aidha, mtu anapofariki chini ya uangalizi wa mamlaka za serikali, kwa mfano Polisi, au Magereza, Jeshi, au penye matokeo ya utekelezaji wa hukumu ya kifo.

Kadhalika mtu anayefariki au anayekutwa kafariki katika mazingira yanayohitaji uchunguzi.

### HATUA YA UCHUNGUZI

Kuna swali linaloibuka ni wakati gani uchunguzi wa kifo unafanyika? Kimsingi, hufanyika pale Korona atakapopokea taarifa na kujiridhisha kuwa kuna mwili wa marehemu kwenye eneo lililoko penye mamlaka yake.

Hiyo, huendana na kuwapo sababu za kuhisi kuwapo mazingira ya kifo hicho, yanayohitaji uchunguzi. Kwa mazingira haya Korona atatakiwa kufanya uchunguzi wa kifo haraka, kwa mujibu wa sheria hiyo.

Vilevile, mamlaka kama polisi, inaweza kutoa maoni kulingana na mazingira ya kifo cha mtu husika na namna ilivyotokea ndani ya mamlaka ya Korona au vinginevyo, mfano kutokuwa na taarifa ya kifo hicho.

Mamlaka hiyo, kiutaratibu inaandika barua na kumtaka Korona afanye uchunguzi wa kifo.

### NAFASI YA MAHAKAMA

Swali lililopo, je Mahakama ya Korona ina mamlaka na wajibu gani? Hapo kuna suala la kuagiza uchunguzi wa kitaalamu wa mwili au postmortem examination, utakaofanywa na daktari wa serikali, kupata taarifa za kitaalamu lengo ni kupata ufafanuzi wa kiuchunguzi kuhusu mazingira ya kifo hicho.

Mamlaka hiyo, pia ina haki ya kuamuru kuzikwa au kuchomwa mwili huo hadi kuwa majivu. Pia, mamlaka hiyo ina haki ya kutoa amri kufukuliwa mwili wa marehemu, uliokwishazikwa.

Lengo hapo linatajwa kuwa ni kufanya uchunguzi (exhumation) na baada ya hapo, inatoa maelekezo ya kuuzika tena.

Pia, Mahakama ya Korona ina mamlaka ya kufanya uchunguzi kwenye kifo kilichotokea ghafla, kwa ajali, kifo cha kikatili au mazingira yanayotiliwa shaka.

Eneo lingine katika orodha hiyo, inagusa vifo vya mwili uliokutwa au ulioletwa ndani ya mipaka ya nchi, Korona atakapoona kuwa ni lazima uchunguzi ufanyike, atafanya uchunguzi juu ya sababu na mazingira yanayohusiana na kifo hicho.

Pale Korona atakapoona hana sababu za kuchunguza ili kubaini sababu na mazingira ya kifo atawasilisha nyaraka na ushahidi unaohusiana na kifo hicho kwa Mkurugenzi wa Mashataka (DPP).

Kisheria mwandishi, anaainisha mfano wa vifo vilivyotokea hivi karibuni na taarifa zake zikionesha ukatili mfano, 'mama na mtoto waliouawa mkoani Dodoma, kada wa CHADEMA, Ally Mohamed Kibao na kifo cha daktari Dismas Chami, kilichotokea mkoani Tabora na mwili wake kutupwa.

Vyote kimsingi vinaangukia mazingira kama hayo na vilipaswa kuchunguzwa na Mahakama ya Korona.

### UNAPOKUTA MAITI

Unapokuta mwili wa marehemu sehemu fulani au kusikia taarifa za kifo, ambazo kimazingira zinahitaji uchunguzi, unatakiwa kutoa taarifa kwa mamlaka kadhaa.

Kwanza Korona, Polisi ili kupeleka taarifa kwa Korona kwa ajili ya uchunguzi.

Kuna kesi zinashindwa kufikia mwisho unaojitosheleza, kwa sababu ushahidi wa kuwatia

INAENDELEA UK. 14

# Wasomi wanavyomuunga mkono Rais wakihubiri nishati safi, ulinzi hifadhi

**Na Christina Mwakangale**




Watalii ndani ya Hifadhi ya Misitu ya asili Kazimzumbwi. **PICHA: MTANDAO**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anahamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia akiwa kinara mtetezi wa kuachana na upishi wa kuni, mkaa na samadi zinazoathiri afya.

Tafiti za matumizi ya nishati zinaonyesha kuwa asilimia 80 ya Afrika inatumia nishati isiyo safi jikoni na kwa Tanzania ni asilimia 90 inatumia nishati isiyo chafu kupikia.

Rais Samia anasema mbali na vifo, nishati chafu inaathiri kimazingira, wanawake na mabinti hutumia muda mwingi kutafuta kuni na mkaa badala ya shughuli nyingine, hivyo anadhamiria kuwaondoa Watanzania katika changamoto hiyo.

Tanzania Landscapes Restoration Organization (TaLRO), ni taasisi inayoanzisha juhudi za kuunga mkono kazi za Rais Samia kulinda mazingira na kutumia nishati safi, kwenye hifadhi za misitu.

Dk. Elikana Kalumanga, mshauri wa asasi hiyo, anazungumza na Nipashe, akifafanua jukumu hilo kuwa mradi unalenga mambo kadhaa mojawapo kupanda miti ya asili 10,000.

Anataja hifadhi ya msitu wa Kazimzumbwi ulioko Kisarawe mkoa wa Pwani, ambao kwa miezi sita watapanda miti hiyo.

Aidha TaLRO kwa kushirikiana na NMB, itaimarisha uchumi wa wanajamii vikiwamo vikundi vya kuweka na kukopa wakiwahusisha wafuga kuku na nyuki.

"Mradi utawashirikisha wanakijiji cha Maguruwe wilayani Kisarawe, kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) kupitia miradi midogo chini ya mfuko wa mazingira."

Dk. Kalumanga anasema: "Asasi hii ilianzishwa na vijana waliomaliza chuo kikuu mwaka 2019 wakishirikiana na walimu wao wakilenga kuondoa dhana ya kuwa wanapomaliza vyuo lazima wawe na uzoefu wa miaka kadhaa. Ukiangalia uzoefu anaupata wapi wakati ametoka kumaliza chuo?"

Anasema wazo likaibuka kwamba walimu waanzishe taasisi ambayo itahifadhi mazingira, ili waliokuwa wanasoma wayafanye mazoezi na kazi kwa kujitolea lakini kwa ufanisi zaidi.

Anasema waliamua ofisi iwe Kisarawe kwa sababu ni eneo lenye msitu wa asili wa Kazimzumbwi moja ya eneo lenye bayoanuwai nyingi duniani.

"Ni kama misitu ya Usambara na Uluguru. Kazimzumbwi una eneo na visehemu yenye umuhimu na hadhi kama msitu wa Amazon," anasema Dk. Elikana.

Anasema Kazimzumbwi ni miongoni mwa maeneo makubwa 25 duniani yenye umuhimu mkubwa wa bayoanuai.

"Unapotaja maeneo manane Afrika yenye baioanuwai kubwa hiyo misitu inayoitwa (coastal east Africa), Kazimzumbwi ipo kwenye hayo maeneo na unaijumuisha kwenye maeneo hayo manane.

Anasema kwa hiyo wakaona ni vyema akaonyesha utaalamu kwa kushirikiana na serikali na baadhi ya wadau wa mazingira kurudisha uhalisia kwa kupanda miti ya asili eneo hilo.

> "Ulinzi wa misitu ya asili ni muhimu lakini mtu anakata miti maeneo ya hifadhi kutokana na kukosa elimu pia kwa sababu uchumi wake ni duni, atapikia nini? Hawezi kumudu gharama ya nishati mbadala kama gesi," anasema.

Anaongeza kuwa hawapandi misitu isiyo ya asili na ikitokea labda miti ya matunda na mbao, itapandwa maeneo ya mwananchi mmoja mmoja kama nyumbani ili kuongeza kipato cha familia.

**MALENGO NA ELIMU**

Dk. Elikana anasema jamii lazima ielimishwe na kubadili dhana kuwa maeneo yaliyohifadhiwa ni kwa ajili ya Wakala wa Misitu (TFS) au Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

"Mfano kwa siku Dar es Salaam inahitali lita milioni 500 za maji na DAWASA inachofanya ni kusambaza na si kuyazalisha yanatoka kwenye maeneo yaliyohifadhiwa kutoka milima ya Uluguru.

"Kila mmoja anapambana apate mboga za majani Dar es Salaam, lakini wakulima wa pembezoni wanategemea mito midogo inayopita pembeni na uhai wa hayo maji kwa Dar es Salaam yanatoka Kazimzumbwi." Anakumbusha.

Anafafanua zaidi kuwa vyanzo vingi vya maji Dar vinatokana na maeneo hayo kwa hiyo umuhimu wake mkubwa na si kwa ajili ya TFS au TANAPA.

Anakumbusha kuwa pakiharibika mfanyakazi wa TFS akiharibu atahamishiwa sehemu nyingine na kuendelea kupokea mshahara wake kama kawaida, lakini wana Dar es Salaam hasa Kisarawe, wataishi kwa taabu.

Anasema utunzaji wa maeneo yenye misitu ya asili una uhusiano mkubwa na uchavushaji wa mazao na hata maua ya aina tofauti.

"Ukiona mtu kazalisha mahindi na kuvuna kuna viumbe wamehusika kuchavusha na sisi tunachukulia kawaida kuwapoteza hao viumbe. Tuwajali."

Anasema ukifika Ujerumani, Uholanzi, Uingereza na Canada wizara zao zinaagiza nyuki na vipepeo kwa ajili ya kuchavusha mazao akiwataka Watanzania kubadilika.

Anaeleza kuwa kwa nchi maskini ni gharama kubwa, lakini kinachoweza kusaidia ni kufanikisha kuzaliana viumbe hao katika misitu ya asili kwa jamii kushiriki kuhifadhi na kama haitashiriki ijue faida zake.

Mradi huo anasema unalenga kuwainua wanawake na vijana kwa kupatiwa elimu ya kutafuta fedha, kuweka na kukopa kutoka Benki ya NMB.

"Tunashirikiana na Benki ya NMB Kisarawe tuanze kusaidia wananchi kuhusu elimu ya fedha na mikopo halafu waweze kupata mikopo nafuu na tuwasaidie kuanzisha shughuli za uhifadhi mfano miradi ya kuku, nyuki na utalii hasa kwa vijana wadogo waanze kuzifanya hasa Maguruwe, Kisarawe na vijiji vya Kazimzumbwi."

Anasema pia mradi utajielekeza kupitia hiyo misitu kutengeneza 'living laboratory' yenye data kamili, mfano mtoto anapoona kipepeo kinavyokua kuanzia funza anayemaliza mazao shambani hadi anakua kipepeo inatakiwa aelewe na aone mchakato.

Mkazi wa kijiji hicho, Shaban Said, anasema anatarajia mradi huo utabadili maisha ya wanavijiji hasa kuondokana na matumizi ya mkaa na kuni ambayo ni chanzo cha uharibifu wa mazingira.

"Ulinzi wa misitu ya asili ni muhimu lakini mtu anakata miti maeneo ya hifadhi kutokana na kukosa elimu pia kwa sababu uchumi wake ni duni, atapikia nini? Hawezi kumudu gharama ya nishati mbadala kama gesi," anasema.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Msimbu, Huruma Jacob, anasema mradi huo utawaimairisha wananchi kimapato kwa kuwa utakuwa endelevu.

Awali, akizindua mradi huo Katibu Tawala wa Wilaya ya Kisarawe, Bupe Mwakibete, anasema mradi huo unaunga mkono juhudi za serikali katika ulinzi wa mazingira ikiwamo kupanda miti.

TaLRO, ni asasi ya kiraia inayofanya kazi za kuhifadhi maliasili kwa kushirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo jamii zinazozunguka maeneo yaliyohifadhiwa mfano misitu ya Kazimzumbwi.

TaLRO inasisitiza kuwa uhifadhi endelevu unahitaji ushiriki wa jamii na zinufaike na faida za hifadhi, kama vile miradi ya jamii katika kukuza kipato cha kaya na cha mtu mmoja mmoja.

# Kongamano Ekaristi Takatifu liwe somo kulinda haki, amani na demokrasia

**Na Mwandishi Wetu**

KENGELE ya wito wa kudumisha amani, umoja, maelewano na mapatano imepigwa na Kanisa Katoliki, ikihimiza na kukumbusha taifa kuthamini zawadi kuu ya uhai na kuendeleza mshikamano wa udugu wa Watanzania.

Jukumu kubwa ni la viongozi wa vyama vya siasa kutimiza wajibu ili kuliweka taifa pamoja ndani ya ramani ya kisiwa cha amani na utulivu na mhifadhi wa kila raia bila kujali kabila, dini itikadi wala mtizamo.

Kanisa kuwakutanisha wanasiasa na viongozi mbalimbali kutoka serikalini na upinzani , kuwe njia ya kufungua pazia na kuingia kwenye barabara itakayoiweka pamoja Tanzania Bara na Visiwani kabla na baada ya uchaguzi wa serikali za mitaa na ule mkuu wa 2025.

Wito wa Kongamano la Ekaristi ni 'udugu wa kuponya ulimwengu' lakini uwe udugu kuiponya Tanzania , ukiwakumbusha pia viongozi wa kijamii, dini,wasomi wanataaluma wa kila aina na mashirika ya kiraia kuwa wadau wa kuhubiri umoja na amani ya taifa .

Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, Katibu Mkuu wa chama hicho John Mnyika na Katibu Mkuu wa CCM Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi wanakutana na kutazamana ana kwa ana wakiwa kwenye kongamano hilo la tano la Ekaristi Takatifu katika Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam, ushirikiano huo uendelezwe kwa manufaa ya kila mmoja.

Wameitwa, wameitikia wito. Hawakupuuza bali walisimama mbele ya halaiki ya waamini wengine wakiwa pamoja kwenye ibada na mbele ya Mungu kuonesha utayari wa kushirikiana.




Katibu Mkuu CCM, Dk. Emmanuel Nchimbi, akimsaidia Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Bara, Tundu Lissu kupanda jukwaani, katikati ni John Mnyika, Katibu Mkuu CHADEMA, wakishiriki Kongamano la Ekaristi Takatifu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Uamuzi huo si mdogo wala si wa kupuuzwa tena si wa kubahatisha .Badala yake wamethibitisha kiapo chao katika dhima ya kusimamia ustawi wa maendeleo ya amani ,utulivu, kuthamini utu na upendo.

Hatua ya kukutanishwa kwao ni wito wa moja kwa moja katika kuonesha kutii mbele ya jamii inayowatazama wakiwa viongozi na wanaotegemewa na wananchi kuwaongoza katika njia inayonyooka na inayojali haki za wote.

Viongozi hao kukutana katika ibada moja,haitokani na nguvu au ujanja wao bali ni karama toka kwa Mungu, inayoelekeza wito wa kuwataka kuepusha aina zote na majanga yanayotishia hatma bora ya taifa.

Kongamano hilo liwakumbushe wanasiasa na raia kuwa kauli mbiu kama tunahitaji ' watu, ardhi, siasa safi, uongozi bora, maendeleo ya uchumi, ustawi wa demokrasia ,utawala wa sheria au kuenzi haki za binadamu ili tuendelee havitafikiwa ikiwa amani itapuuzwa , kuchezewa na kuachwa itoweke.

Popote duniani amani, utulivu na umoja vilipokosekana kilichotawala ni shari, kuporomoka maadili, chuki , kukosa maelewano, vita, kumwaga damu, uasi na vifo vinavyoondoa zawadi kuu ya uhai ambayo ni haki ya msingi ya binadamu.

Watanzania wakumbuke kuwa haipo nchi yoyote duniani iliyofuzu kama haikuenzi amani na umoja wa kitaifa, kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria.

Tanzania iliyojenga na kudumisha umoja wake, udugu wa watu wake bila kutumia nguvu na ushawishi wa ukabila ,dini, rangi au ukanda, haipaswi ikubali ipoteze tunu ya mshikamano wake kwa sababu yoyote.

Kengele iliyopigwa kwenye kongamano la tano la Ekaristi Takatifu imewajumuisha wanasiasa kwa niaba ya vyama na wafuasi wao.Viongozi wa vyama vikuu CCM na CHADEMA wakisimama bega kwa bega mbele ya viongozi wa dini yote hiyo ikionesha njia ya muafaka.

Kusimama kwao kuwe mwanzo wa kuelekea katika maelewano thabiti na kutuma ujumbe utakaodumisha amani badala ya kutokea vurugu, chuki na hamaki na wakati mwingine habari za mauti.

Siku zote jazba, chuki, husuda na hamaki hazijajenga badala yake vitu hivyo vinadhoofisha hupoteza uhai na maisha ya watu, kuvuruga amani ,maelewano , maendeleo ya kisekta na kuwarudisha nyuma watu na taifa wakibakia masikini tena wanaosongwa na migawanyiko.

Historia siku zote ni mwalimu, Tanzania bila amani isingefanya lolote katika harakati za kujenga nchi, kupigania uhuru wake na kufanikisha ukombozi Kusini mwa Afrika na kuhifadhi wapigania uhuru wa kila pembe ya dunia .

Vyama kadhaa vya wapigania uhuru viliendeleza harakati zake katika ardhi ya Tanzania ili viweze kupigania uhuru, kutafuta haki ,usawa na umoja katika nchi zao na leo Msumbiji, Angola, Zimbabwe, Afrika Kusini ni huru.

Katika vipindi hivyo vyote Tanzania ilikabiliana na mitikisiko, misukosuko ya ndani na nje, shida,vita na Uganda, furaha na misiba lakini imeendelea kuwa kisiwa cha amani na utulivu kutokana na taifa kuwa na umoja , amani, utulivu na mshikamano wa kindugu.

> Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lissu, Katibu Mkuu wa chama hicho John Mnyika na Katibu Mkuu wa CCM Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi wanakutana na kutazamana ana kwa ana wakiwa kwenye kongamano hilo la tano la Ekaristi Takatifu katika Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam, ushirikiano huo uendelezwe kwa manufaa ya kila mmoja.

Licha ya kuwepo taabu , dhiki na hata upungufu wa baadhi ya bidhaa na huduma muhimu za kufanikisha maisha, Watanzania walibaki wamoja katika nyakati zote hatimaye kupata ushindi wakishikamana hivyo hata sasa amani hiyo iendelezwe kwa juhudi zote.

Sauti na wito kutoka katika kongamano hilo ni sauti muhimu kusikilizwa . Ni ujumbe wa amani wala si utani au mzaha bali ni wazi viongozi wa vyama vya siasa wanatakiwa kukutanishwa pamoja mezani kujadili hatma ya nchi hasa kudumisha amani ushirikiano na umoja pia kudumisha demokrasia na uhuru ambavyo ni haki ya kila mmoja.

Viongozi wa dini wameonesha njia ya kujenga demokrasia na misingi ya utawala bora kwa vyama vya siasa kushindana kwa hoja pamoja na dhamana ya kusimamia kwa vitendo usalama wa raia, uhai wao na mali zao, kujenga uchumi na kujiepusha na sintofahamu zinazojitokeza na kutia doa historia ya taifa hilo linalotukuka kwa amani na kushikamana.

JUKWAA LA VIONGOZI



Kamala Harris



Donald Trump

# Ndivyo wagombea urais Marekani walivyochuana

## •Mwonekano Trump ukali, Kamala sura ya mshangao

**Na Mwandishi Wetu**

DONALD Trump na Kamala Harris wametunishiana misuli kwa mara ya kwanza kwenye jukwaa la mdahalo wa urais huko jijini Philadelphia.

Wanaofuatilia mchuano huo wapo wanaoweza kumwita mgombea wa Democrat Kamala Harris 'the sleeping giant.' Wakati Mzee Trump akibaki na viulizo.

Ikimaanisha kuwa ana nguvu lakini bado hajaonyesha kiwango kamili cha uwezo wake.

Katika dakika 90 za patashika, Harris mara kwa mara alimvaa rais mstaafu Donald Trump kwa mashambulizi binafsi ambayo yalimtoa Trump kwenye mstari ni kwa mujibu wa BBC.

Harris anazungumzia mwenendo wa Trump wakati wa ghasia za Capitol au jengo la bunge na maofisa waliohudumu katika utawala wake ambao wamekuwa wakosoaji wa wazi wa kampeni zake mara kwa mara, akimuacha Trump katika wakati mgumu.

Sehemu kubwa ya mdahalo huu, Harris alimweka mpinzani wake wa Republican katika mazingira ya kutoa utetezi kuhusu mwenendo na maoni yake ya zamani.

Wakati mwingine Trump akalazimika, kupaza sauti yake mara kwa mara na kutikisa kichwa, inaeleza BBC.

"Wamarekani wanapaswa kwenda kwenye mkutano wa Trump," Harris anasema wakati wa swali la mapema kuhusu uhamiaji. "Watu huanza kuondoka kwenye mikutano mapema kutokana na uchovu na kuchoka," anasema.

Shambulizi hilo ni wazi lilimkera rais huyo wa zamani, akatumia sehemu kubwa ya jibu lake - kwenye mada ya uhamiaji ambayo ni moja ya eneo kuu la nguvu, kutetea ukubwa wa mikutano yake na kudharau kampeni za Harris.

Trump anakwenda mbali zaidi hadi katika ripoti iliyokanushwa kwamba wahamiaji wa Haiti katika mji wa Springfield jimboni Ohio, walikuwa wakiteka nyara na kula wanyama wanaofugwa sehemu hiyo.

Iwapo midahalo ina kushinda na kupoteza, ni mgombea yupi anayetumia vyema masuala ambayo yanampa nguvu na kutetea hoja au kukwepa maeneo yenye udhaifu kwake, kilichofanyika Jumanne iliyopita usiku utasema ulikuwa ni wakati wa Makamu wa Rais Kamala, inasema BBC.

Katika mada za uchumi na kutoa mimba zilipojadiliwa, uchunguzi wa maoni ya umma unaonyesha Wamarekani wengi hawajafurahishwa na jinsi utawala wa Biden ambao Harris ni mwanachama muhimu ulivyoshughulikia mfumuko wa bei na uchumi.

Lakini Harris anageuza mada hiyo na kuzungumzia ushuru uliopendekezwa na Trump, na kuuita ni "kodi ya mauzo ya Trump" na kisha akaleta mradi wa 2025, mpango huru wenye utata wa utawala wa baadaye wa Republican.

Kama ilivyokuwa huko nyuma, Trump anajitenga na mradi huo na kutetea mpango wake wa ushuru, akibainisha kuwa utawala wa Biden ulikuwa umeweka ushuru mwingi katika muhula wake wa kwanza wa urais.

Zilikuwa hoja halali, lakini zilimzuia kumkosoa Makamu wa Rais kuhusu mfumuko wa bei na ugali wa bidhaa, inaeleza BBC.

Kuhusu mimba, Trump anatetea jinsi alivyoshughulikia suala hilo, akisema Wamarekani katika nyanja mbalimbali wanataka sheria ya kutoa mimba ya Roe Wade ibatilishwe na Mahakama ya Juu. Kauli ambayo kura za maoni haziiungi mkono. Anahangaika kueleza msimamo wake na jibu lake wakati fulani lililokuwa la kukurupuka.

Kamala, wakati huo huo, anachukua fursa hiyo kutoa kauli ya hisia kwa familia ambazo zimekabiliwa na matatizo ya ujauzito na hazijaweza kupata huduma ya kutoa mimba katika majimbo ambayo yamepiga marufuku utaratibu huo, yenye "marufuku ya Trump ya kutoa mimba".

Kama alivyoyaita Kamala: "Ni matusi kwa wanawake wa Marekani," anahitimisha.

Ni ujumbe uliopangwa kwa uangalifu katika eneo ambalo ana faida kuliko Trump, BBC inachambua.

Wakati mdahalo ukiendelea, Harris anamweka Trump kwenye mashambulizi na kejeli, ambazo angeweza kupuuza lakini inalazimika kuzijibu.

Wakati mmoja, Harris anaulizwa maoni yake ya uchumi aliyo achana nayo zamani, wakati wa kampeni yake ya urais iliyoshindwa 2019.

Rais wa zamani badala ya kumkosoa Makamu wa Rais juu ya maoni yake yanayobadilika, kuonyesha udhaifu wake wa wazi, alifungua majibu yake kwa kuzungumza "sehemu ndogo" ya pesa aliyochukua Kamala kutoka kwa baba yake.

Kuhusu kujiondoa Afghanistan, eneo jingine dhaifu kwa Harris, Makamu wa Rais, anahamisha mazungumzo na kuyapeleka kwenye maelezo ya Trump na maofisa wa Taliban na kuwaalika Camp David, eneo maarufu kwa shughuli za marais wa nchi hiyo.

Ilikuwa ni mbinu ambayo ilijirudia na ilionekana kufanya kazi vizuri.

Wanachama wa Republican tayari wanalalamika kuhusu kile wanachosema ni upendeleo ambao wasimamizi wa ABC, David Muir na Linsey Davis, waliuonyesha kwa Harris. Wote wawili walimrudisha nyuma Trump na kukagua madai ya uongo aliyoyatoa mara kadhaa.

Mwishowe, hata hivyo, yalikuwa ni majibu ya Trump na shauku ya kuchukua na kula chambo chochote ambacho Harris alikiweka katika mdahalo wa jioni.

Wakati wowote mpinzani wa Harris alipokuwa akizungumza, Harris aliweka sura ya mshangao au kutokuamini. Trump, kwa upande wake, sura ya kukasirika zaidi.

Timu ya kampeni ya Harris ilikuwa haijaamua hapo awali ikiwa itakubali mjadala mwingine. Mara tu baada ya huu kumalizika, wanaitisha mjadala wa pili wa urais kabla ya Novemba.

Hiyo pekee inaonyesha jinsi wanachama wa Democratic walivyoona namna Jumanne usiku ilivyokwenda kwa Harris, kwa mujibu wa BBC.

# IMETIMU WAKATI WA KUANZA KUTUMIA MAHAKAMA YA KORONA

**INATOKA UK. 11**

hatiani watuhumiwa haujajitosheleza.

Hiyo ni kwa sababu katika kesi hizo, huenda uchunguzi ulipwaya, wakati mkondo wa uchunguzi wa Korona, ungejitosheleza zaidi.

Ingawa kuna sheria mahsusi inayotambua Mahakama ya Korona, lakini mara nyingi haitumiki na kazi zake zinafanywa na mamlaka nyinginezo.

**MAONI YA UMMA**

Vilevile mahakama hiyo haifahamiki kwa wengi, bali kundi kubwa wanachofahamu ni kesi zote huchunguzwa na polisi.

Anashuhudia Denis Kitandala, mkazi wa Mwanza, anayesema 'hajawahi kuisikia wala kuiona Mahakama ya Korona,' bali anazozijua ni Mahakama ya Mwanzo, Wilaya na Mahakama Kuu.

Anaendelea kusema kuwa anafahamu matukio ya mauaji na kesi zote huchunguzwa na polisi na hatambui chombo kingine chenye mamlaka ya kuchunguza ama kifo au vifo.

Mtazamo wa Deborah Mwakiposa mkazi wa Kinondoni, Dar es Salaam, ni haijui kwa kina Mahakama ya Korona na mtazamo wake wa awali ni kwamba "mahakama inayohusika na kesi zinazohusu ugonjwa wa COVID 19 au UVIKO 19."

Mwanasheria, Manoni Makoye, mkazi wa Dodoma, anasema aliwahi kuisoma

kwenye vitabu vya sheria, lakini hajawahi kuiona mahakama hiyo au kuwaona makorona

kwenye tukio la kifo tatanishi wakifanya uchunguzi.

Nchi zilizoendelea, kuna Mahakama mahusus za Korona kisheria na zimekuwa zikiwasaidia kubaini sababu na mazingira ya vifo vya kutatanisha.

Mitazamo na yanayojiri nchini, ni fursa kwa wanasheria kuishauri serikali kuimarisha Mahakama ya Korona nchini, ili ifanye kazi kwa mujibu wa sheria, kusaidia kupatikana haki na amani.

Pia, mahakama hiyo inapaswa kuwa na majengo yake, ndani yake ikijumuisha wataalamu waliobobea kwenye sheria, pia uchunguzi na uhalifu.

Ikiwa na mfumo huo katika ngazi ya kila wilaya itakuwa bora zaidi, ili kurahisisha wananchi kuwasilisha taarifa za vifo moja kwa moja kwenye mamlaka husika.

Hiyo ikifanyika na kutolewa elimu ya umma kuhusu majukumu yake, inakuwa ushindi katika kuifanikisha haki na utawala bora kwa maslahi ya umma.

**Ni maoni binafsi ya mwandishi ambaye ni wakili. Kwa maoni simu: 0759447946, joranherman95@gmail.com**





# INEC: Mawakala wa vyama msiwaingilie watendaji

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TUME Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), imewataka mawakala wa vyama vya siasa kutowaingilia watendaji wakati wa uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura vituoni.

Mjumbe wa Tume hiyo, Dk.Zakia Abubakar, alitoa rai hiyo juzi wakati akifungua mafunzo ya uboreshaji wa daftari hilo yaliyoshirikisha maofisa waandikishaji, maofisa waandikishaji wasaidizi ngazi ya jimbo, maofisa uchaguzi, maofisa ugavi na maofisa TEHAMA wa Halmashauri.

Alisema wakati wa uboreshaji wa daftari mawakala wa vyama vya siasa wataruhusiwa kuwapo katika vituo vya kuandikisha wapigakura ili kuleta uwazi katika zoezi hilo.

"Mawakala hao watasaidia kutambua waombaji wa eneo husika na hivyo kupunguza kutokea kwa vurugu zisizokuwa za lazima, lakini hawaruhusiwi kuwaingilia watendaji wakati wakitekeleza majukumu yao vituoni," alisema.

Alisema tume ilishatoa kibali kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uboreshaji wa daftari kwa asasi za kiraia 157 na asasi nyingine 33 zitahusika kwa ajili ya uangalizi wa zoezi hilo.

**"Mawakala hao watasaidia kutambua waombaji wa eneo husika na hivyo kupunguza kutokea kwa vurugu zisizokuwa za lazima, lakini hawaruhusiwi kuwaingilia watendaji ...**

"Ni muhimu kutoa ushirikiano kwa asasi hizo zitakapofika kwenye maeneo yenu kwa ajili ya kutekeleza majukumu yao ambapo tume itawapa vitambulisho kwa urahisi wa kuwatambua," alisema.

Abubakar alisema maofisa hao wahakikishe wanatekeleza majukumu yao kwa umakini katika kila eneo ikiwemo utunzaji wa vifaa vya uandikishaji kwani vifaa hivyo vimenunuliwa kwa gharama kubwa sana.

Alisema matokeo bora ya zoezi la Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura yanategemea uwepo wa ushirikiano mkubwa kati ya watendaji wa serikali, vyama vya siasa na wadau wengine wa uchaguzi.

"Niwasihi muwe na ushirikiano mzuri na wa karibu na tume wakati wote wa mtakapokuwa mnatekeleza majukumu yenu na ikiwa mnahitaji ufafanuzi wa maelezo yoyote msisite kuwasiliana na tume," alisema.

Mafunzo kwa maofisa hao yalihusu namna ya utunzaji wa fomu pamoja na kutumia mfumo wa kuandikisha wapigakura (VRS), kwa upande wa maofisa TEHAMA walipewa mafunzo maalum ya jinsi ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiufundi endapo zitajitokeza wakati wa zoezi la uandikishaji wapigakura vituoni.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, akizungumza na wafanyabiashara wa Soko la Machinga, wakati wa mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero mbalimbali. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Kaya 900 Singida hazina vyoo

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

KAYA zaidi ya 900 kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Singida hazina vyoo na wamekuwa wakijisaidia kwa majirani.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida, Joanfaith Kataraia aliyasema hayo alipokuwa akizungumzia hali ya uzalishaji wa taka ngumu na maji taka katika Halmashauri hiyo kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2024.

Alifafanua kuwa kaya hizo ni kati ya zaidi ya kaya 500,000 zilizokuwapo kwa kipindi hicho.

"Katika kipindi cha mwaka 2021 kulikuwa na kaya 107,790 huku kukiwa na kaya 819 zisizokuwa na vyoo wakati mwaka 2022 kulikuwa na kaya 110,920 na kati ya hizo kulikuwa na kaya 170 zisizokuwa na vyoo, mwaka 2023 kulikuwa na kaya 142,173 na mwaka 2024 kulikuwa na kaya 164,091 lakini hapakuwa na kaya zisizokuwa na vyoo,"alisema.

Kataraia alisema halmashauri hiyo inazalisha taka ngumu na taka maji na wastani wa tani 140 kwa siku na kati ya hizo tani tano ni chupa za plastiki na kwamba wametenga maeneo maalumu ya kutupa taka, hususani kwenye maeneo ya masoko kwa muda kabla ya kuzipeleka dampo kuu lililopo Kijiji cha Mwankonko.

"Kwa sasa Halmashauri ina utaratibu wa kupitisha magari ya taka katika ngazi ya kaya, biashara pamoja na taasisi kuchukua taka na kuzipeleka dampo kuu,"alisisitiza.

Ofisa Mazingira wa Halmashauri hiyo, Theresia John alifafanua kuwa kupitia kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira, hutumia mbinu mbalimbali ili kudhibiti mlipuko wa magonjwa yatokanayo na uchafuzi wa mazingira.

Theresia alizitaja mbinu hizo kuwa ni kuhakikisha kila kaya inajenga choo bora na kukitumia, kutembelea kaya kwa kaya ili kuhakikisha zinajenga choo bora na kukitumia na kutoa elimu ya afya kwa kila kaya dhidi ya matumizi bora ya vyoo.

Ofisa Mazingira huyo alisema katika utekelezaji wa Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2019 watu 245 walitozwa adhabu ya faini ya sh. 50,000 kila mmoja na Sh. milioni 12.25 zilikusanywa.

# Wawekezaji waitwa kuwekeza Ruvuma

**Na Augusta Njoji**

WITO umetolewa kwa wawekezaji nchini kuchangamkia fursa ya kuwekeza mkoani Ruvuma kutokana na kuwapo na vivutio mbalimbali, ikiwamo kaburi la chifu wa wangoni aliyezikwa na wasaidizi wake wawili wakiwa hai.

Chifu huyo aliyefahamika kwa jina la Nkusi Mharule bin Zulu Gama alitawala wangoni mwaka 1874-1889.

Akizungumza jana mkoani humo katika kuelekea Tamasha la Tatu la Kitaifa la Utamaduni, Msimamizi wa eneo hilo la utalii, Agnes Ngonyani alisema katika kaburi hilo amekuwa akipokea wageni kutoka maeneo mbalimbali duniani kwa ajili ya kuzuru.

"Katika eneo hili zimetengwa heka nane tunawakaribisha wawekezaji kupitia Rais Samia Suluhu Hassan waje kuwekeza eneo hili kwa kufanya mambo mbalimbali ya kuinua mila na desturi zetu zilizoachwa na mababu zetu,"alisema.

Alisema kwa tamaduni zao kila mwaka wangoni wamekuwa wakihiji kwenye kaburi hilo kuomba baraka kwa kiongozi wao.

"Katika kaburi hili huyu chifu alizikwa na watu wawili wakiwa wazima na hao watu walikuwa wasaidizi wake na wala hawakukamatwa kwa ubabe waliambiwa wewe na wewe tunakwenda kuwazika pamoja na chifu na walipopewa ujumbe huo walifurahia ni jambo jema kuzikwa na chifu."

"Umaarufu wa kaburi hili pia kuna nyoka mkubwa haonekani mara kwa mara, baada ya miaka mitano au 10 huenda huko bondeni kunywa maji. Mimi hadi umri huu sijawahi kumuona ila kuna watu wameshawahi kubahatika kumuona," alisema.

Makamu Mkuu wa Shule ya Sekondari Jenista Mhagama, Meliud Mwampembe, alisema shule hiyo imetoa kipaumbele kwa masuala ya michezo na utamaduni kwa wanafunzi.

"Hili jambo la utamaduni na michezo ni la msingi kwa sababu linatunza asili yetu sisi kama Watanzania, ninahamasisha sana wananchi kushiriki katika tamasha hili linaloonesha tamaduni zetu lakini na fursa mbalimbali zilizopo Ruvuma,"alisema.

Tamasha hilo litafanyika kwa siku tatu kuanzia Septemba 20 hadi 23 mwaka huu na Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye kilele.



# Ujenzi barabara Luvulunge-Kwakavuta waiva

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WAKALA wa Barabara Mjini na Vijijini TARURA Wilaya ya Makete umesema Septemba 24 mwaka huu, utaanza ujenzi wa Barabara ya Luvulunge hadi Kwakavuta (km 25), ili kuokoa maisha ya wajamzito na watoto pindi wanapotafuta huduma za afya.

Mhandisi wa TARURA, Frank Kapesa alieleza hayo juzi wakati wa uzinduzi wa Zahanati ya Kijiji cha Ivilikinge iliyokwenda sambamba na hafla ya kukabidhi vifaa tiba, ikiwamo vitanda kutoka Benki ya NMB vyenye thamani ya Sh.milioni tisa.

Kapesa alisema barabara hiyo imepata fedha za aina mbili ambapo awamu ya kwanza ni kutoka Luvulunge hadi Ivilikinge na awamu ya pili ni Ivilikinge hadi Kwakavuta, ambapo miradi hiyo itatekelezwa kwa fedha za dharura.

Alisema wanategemea barabara hiyo ianze kujengwa wiki ijayo, kwamba mkandarasi atakuwa eneo la mradi kuanza kutekeleza kazi zake.

Kaimu Meneja Benki ya NMB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Willy Mponzi, alisema benki hiyo kila mwaka imekuwa na utamaduni wa kutenga asilimia moja ambayo inarudi kwa jamii. "Msaada huu ambao leo tumekabidhi Makete pia tumekuwa tunakabidhi katika sehemu mbalimbali katika nchi yetu na huu msaada umehusisha vifaa tiba," alisema Mponzi.

**"Msaada huu ambao leo tumekabidhi Makete pia tumekuwa tunakabidhi katika sehemu mbalimbali katika nchi yetu na huu msaada umehusisha vifaa tiba," alisema Mponzi.**

Naye Katibu wa Chama cha Maendeleo Makete (MDA), Award Mpandila, aliishukuru NMB kwa msaada huo na kueleza kuwa kuna umuhimu wa kujenga barabara kwa sababu itasaidia wananchi kupata huduma ikiwamo za afya na kusafirisha mazao yao ili kwenda sokoni.

Kwa upande wake, Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana, alisema serikali itaendelea kuhakikisha huduma mbalimbali zinaendelea kuwafikia wananchi.

"Tumeshuhudia katika wilaya yetu, madarasa yanaendelea kujengwa kwa ajili ya huduma za elimu, tumeshuhudia barabara wilaya hadi wilaya na serikali imetambua barabara," alisema Dk. Chana.

Dk. Chana alisema ujenzi wa barabara katika kijiji hicho ni muhimu kwa sababu ni kichocheo cha maendeleo kwa sababu itasaidia pia kusafirisha mazao yao.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Kijiji cha Ivilikinge, Hassan Yusuph, alisema wakati wa utekelezaji wa mradi huo walikuwa wanakabiliwa na tatizo la ubovu wa miundombinu ya barabara.



Mkuu wa Operesheni wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, ACP Nassor Sisiwaya (kulia) na askari wengine wakiwa katika usimamizi wa Sheria ya Usalama Barabarani, eneo la Mafinga, wilayani Mufindi, mkoani Iringa juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC awaomba viongozi wa dini kukemea uvunjifu wa amani

**Na Agustino Kihombo,** IRINGA

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Kheri James amewaomba viongozi wa dini wilayani humo kuongeza nguvu katika kukemea na kupiga vita vitendo vinavyoashiria uvunjifu wa amani pamoja na mmomonyoko wa maadili.

Alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na viongozi wa dini katika kikao maalum cha kujadili masuala mbalimbali ikiwamo suala la maadili na malezi mkoani hapa.

Pamoja na mambo mengine aliwaomba viongozi wa dini kusimama kidete katika nafasi zao kufundisha waumini wao namna wanavyoweza kuishi kwa kuukataa ubaya.

Alisema serikali inatambua kazi kubwa inayofanywa na viongozi wa dini katika kuirekebisha jamii kupitia mafundisho mbalimbali wanayoyatoa.

"Nimeona nikutane na nyie kama viongozi wa dini ili tukumbushane mambo kadhaa yanayoihusu jamii yetu ya Iringa, miongoni mwa mambo hayo ni pamoja na kuwashukuru kwa kazi mnayoendelea kuifanya ya kuwahudumia wananchi na waumini wenu kiroho, lakini kubwa ni kuwaomba viongozi wa dini mwendelee kuwahubiria waumini wenu kuhusu ulinzi wa amani na mstakabali wa taifa letu," alisema James.

Nao baadhi ya viongozi wa dini walioshiriki katika kikao hicho akiwamo Mchungaji, Nickson Kawage alisema miongoni mwa mambo yanayochangia amani kupotea ni pamoja na watu kukosa hofu ya Mungu.

Alisema: "Ni kweli sisi kama viongozi wa dini tuna mchango mkubwa wa kuhakikisha dunia inakuwa mahali salama pa kuishi, watu waishi kwa misingi ya kimungu na wapendane na kuchukuliana kama ndugu".

# Halmashauri yaanza ujenzi shule mpya

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KATA ya Maguvani Halmashauri ya Mji wa Makambako imeazimia kuanza ujenzi wa shule ya sekondari mpya katika eneo la Mdete lililoko Mtaa wa Sekondari, kutokana na Shule ya Sekondari ya Maguvani kuwa na wanafunzi zaidi ya 1,300.

Hayo yalibainishwa juzi na Diwani wa Kata ya Maguvani ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hanana Mfikwa, wakati akizungumza na wananchi katika mkutano wa hadhara wa Mbunge wa Jimbo la Makambako, Deo Sanga.

Alisema serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) itajenga madarasa matatu, matundu sita ya vyoo na bweni la wasichana kwa gharama ya Sh. milioni 227 ili kuhakikisha mpango huo unafanikiwa.

Mfikwa alisema sababu kubwa ya kuanzisha ujenzi huo ni kutokana na Sekondari ya Maguvani kutakiwa kuwa na kidato cha tano na sita, kueleza kuwa licha ya serikali kutoa fedha katika ujenzi wa shule hiyo pia wananchi watashiriki kwa kutoa nguvu kazi zao, ili ifikapo Januari wanafunzi waanze kuripoti shuleni hapo.

Naye Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Nakembweta Makala, alisema halmashauri kupitia mapato ya ndani imetenga Sh. milioni 10 ili kusaidia ujenzi wa Shule ya Sekondari Mdete.

"Katika bajeti ambayo tunaanza kuitekeleza mwaka 2024/2025 inagharama ya kiasi cha shilingi milioni 424, tuna miradi ambayo tutaanza kuitekeleza, tuna ujenzi wa madarasa matatu na matundu nane ya vyoo katika Shule ya Sekondari Maguvani kwa gharama ya shilingi milioni 91," alisema Makala.

Baadhi ya wananchi wa Kata ya Maguvani akiwamo, Christopher Mepelo, alisema licha ya shule hiyo kwenda kuondoa adha ya baadhi ya wanafunzi kutembea umbali mrefu pia itasaidia kukuza mji hasa katika eneo la Mdete, huku wakitaka kupatiwa ufafanuzi juu ya maeneo yao ambayo shule itajengwa endapo atalipwa fidia.

## ULINGO yapaza sauti matukio utekaji, mauaji

**Na Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Wanawake Viongozi wa Vyama Vya Siasa nchini (ULINGO), umepinga vitendo vya mauaji na utekaji vinavyoendelea nchini.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam katika kuelekea kilele cha Siku ya Amani Duniani itakayofanyika Septemba 21, mwaka huu msemaji wa umoja huo, Saum Rashi, alisema hali ya matukio ya mauaji na utekaji yanayoendelea kwa sasa yanapaswa kukemewa.

Alisema matukio hayo yanaondoa amani ya taifa iliyotunzwa na kulindwa kwa muda mrefu.

Hivyo, aliwataka wanawake kutojihusisha na vitendo vya aina yoyote vya uvunjifu wa amani ili kujitenga na machafuko yanayoweza kuleta hali ya sintofahamu ndani ya jamii.

"Nawasihi wanawake wenzangu msiingie katika mkumbo wowote unaoweza kuligawa taifa letu kwa kuleta uvunjifu wa amani kwani misingi iliyoilea nchi yetu ni muhimu kuitunza kwa gharama yoyote," alisema.

Pia alilaani kitendo cha watu ambao siyo wema kumhusisha na mauaji, Rais Samia Suluhu Hassan katika mitandao ya kijamii, akisema siyo cha kiungwana.

Alisema Tanzania ni kielelezo cha amani katika Ukanda wa Afrika Mashariki, ambapo Rais Samia alichukua hatua muhimu katika kuimarisha maridhiano na mshikamano wa kitaifa kwa kudumisha falsafa yake ya R4.

Kwa mujibu wa Rashi, Rais Samia amefanya mambo mengi ikiwamo ujenzi wa miundombinu, sekta ya utalii na utekelezaji wa masuala ya biashara ambapo amekuwa mfano wa kuigwa nchini na nje ya nchi.

Naye Katibu wa Wanawake wa Chama cha Democratic Party (DP), Neema Mwakitwange, aliwaomba wanawake nchini kutokuwa na lugha chafu dhidi ya Rais Samia na kutokubali kutumika katika machafuko yanayoweza kuchochea vurugu ndani ya nchi.

# Makamu wa Rais aagiza kutengwa rasilimali

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amezitaka wizara na taasisi Tanzania Bara na Zanzibar kutenga rasilimali za kutosha, ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwa serikali zote mbili.

Alitoa rai hiyo jana visiwani Zanzibar wakati akifungua Kongamano la Tatu la Kitaifa la Wiki ya Ufuatiliaji, Tathmini na Kujifunza lililofanyika visiwani Zanzibar.

Alisema serikali imeanzisha idara na vitengo mahsusi vya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

Hivyo aliwataka maofisa masuhuli kuhakikisha vitengo hivyo vinaimarishwa kwa kutenga rasilimali fedha, watu na vitendea kazi vya kuwawezesha kutekeleza majukumu yao na kuendelea kuwajengea uwezo katika eneo hilo.

Pia alizitaka taasisi hizo kuhakikisha taarifa zinazowasilishwa zinatumika katika kufanya maamuzi na kuweka mikakati imara ya kuhabarisha umma juu ya matokeo ya utekelezaji wa kazi za serikali.

Alisema nchi ipo katika mchakato wa kuandaa Dira ya Pili ya Maendeleo ya Taifa itakayoishia mwaka 2050 ambayo ndiyo nguzo kuu inayoainisha mwelekeo wa nchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Bunge na Uratibu, William Lukuvi, alisema katika kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa kikamilifu marais wote wawili wanaendelea kutoa maelekezo na nyenzo za kufanikisha utekelezaji wake kwa ufanisi na ukamilifu kwa wakati na kulinda thamani ya fedha iliyotumika katika miradi hiyo.

Aidha, alisema serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu imetekeleza kikamilifu azimio la kuandaa miongozo mbalimbali ya ufuatiliaji na tathmini.

Alisema miongozo hiyo ni pamoja na, mwongozo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini, miongozo miwili ya usimamizi wa tathmini na mwongozo wa kutathmini utayari wa taasisi katika kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi, alisema ufuatiliaji na tathmini ni dhana muhimu katika kuelezea mafanikio ya utekelezaji wa maendeleo zinazotekelezwa nchini ikiwamo sera, mipango, miradi, programu na mikakati mbalimbali.



Mwakilishi wa Jimbo la Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir, akichangia hoja katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani nje ya mji wa Zanzibar, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yafanya uchambuzi kubaini athari ugonjwa corona

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar imefanya uchambuzi yakinifu wa kubaini athari zilizotokana na ugonjwa wa virusi vya corona, kuathiri sekta ya utalii kwa wageni kushindwa kutembelea visiwa vya Zanzibar kutokana na baadhi ya mataifa kuchelewa kufungua masoko ya utalii nchini kwao.

Waziri wa wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Soraga, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah Ameir aliyetaka kujua ni athari zipi zimejitokeza kutokana na kukosa soko la watalii kutoka nchini Italy.

Waziri Soraga alisema pamoja na athari zilizojitokeza hakujaathiri mwenendo wa soko la watalii wanaotoka Italy kwa kuwa kutokana na takwimu za miaka mitano za watalii hao imeonekana kuongezeka mwaka hadi mwaka. Alisema kwa mwaka 2019 idadi ya watalii 61,315 waliingia Zanzibar kutoka Italy, kwamba kwa idadi hiyo imeifanya kuwa nchi iliyoongoza kuleta watalii wengi nchini.

Alisema mwaka 2020 idadi ya watalii 21,426 wamefika Zanzibar kutoka Italy na kuifanya kuwa ni nchi ya tatu kuleta watalii wake.

Aidha, alisema kwa mwenendo huo unaonesha kuwa wizara kwa kushirikiana na wadau wa utalii imechukua hatua madhubuti ya kuhakikisha soko la utalii kutoka Italy na mataifa mengine linaendelea kukua siku hadi siku.

# 'SJMT, SMZ zinafahamu tatizo biashara usafirishaji binadamu'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) zinafahamu uwepo wa tatizo la biashara ya usafirishaji wa binadamu, ambalo ni tatizo linaloikumba dunia nzima.

Alisema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Mohamed Ali Suleiman, aliyetaka kujua, serikali inalitambua vipi tatizo hilo na ni matukio mangapi ya biashara haramu za binadamu yamewahi kuripotiwa Zanzibar.

Alisema kwa bahati mbaya Zanzibar imekuwa ikitumika kama njia za biashara hiyo, kwa kutumia kipengele cha ajira nje ya nchi ambapo baadhi ya watu husafiri kwa kutumia kisingizio cha ajira bila ya kuwa na mkataba wa ajira uliothibitishwa na ofisi za kibalozi nje ya nchi.

Alisema ni kweli kumekuwa na changamoto ya baadhi ya watu kuletwa Zanzibar kwa ajili ya kuingizwa katika biashara haramu inayodhalilisha utu.

Aidha, alisema kwa kipindi cha Januari hadi Agosti, 2024 Idara ya Uhamiaji ilifanikiwa kuwapata waathirika watatu wa biashara haramu wa usafirishaji binadamu waliorejeshwa nchini wakitokea nchini China.

Alisema katika kuchunguza na kuzuia biashara hiyo haramu, serikali inatumia mfumo wa udhibiti wa mipaka, unaoiwezesha serikali kuweka kumbukumbu za uhalifu na wahalifu wanaovuka mipaka na kuiwezesha serikali kuzuia wahalifu hao kuingia kufanya uhalifu nchini.

Alisema serikali imeanzisha utaratibu maalum wa kutoa ruhusa kwa Watanzania wanaokusudia kufanya kazi nje ya nchi, ambapo wafanyakazi wanatakiwa kuwa na mkataba wa ajira na mikataba hiyo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SALIM ALLY BARUANI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0321/0280** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KINONDONI SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka **2004** . kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi**. POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIG/197524/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERNEST VICTOR MKANWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.2136.0061 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MOUNT IGOVU SECONDARY mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/UBU/198720/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ANASTAZIA RAFAELI PAULO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S/1063-0003 kilichotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia **MULBADAW SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PHQ/ARU/ARU/33571/2024**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**SONGEA LILILOKO SAONGEA**
**MAOMBI NAMBA 61/2024**
**KINDI LUTELEMBA GOGO ——————- MUOMBAJI .**
**DHIDI YA**
**GILE. RUPASA CHUMA**
**ANAF SWALEHE**
**RASHID NCHIMBI**
**ALLY NEBO**
**MOHAMED MPEPO ———————- WAJIBU MAOMBI.**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

Mohamed Mpepo anataarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yenu .Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au Wakili wako ,au wote kwa pamoja siku ya tarehe 01/10/2024 saa 4:00 asubuhi.Shauri linakuja kwa ajali ya kutajwa.

Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako.

Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 16/08/2024.

———————————————————
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)**
**RUVUMA**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EMILIA JEROME MASAWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha Chuo Degree of Insurance and Risk Management chenye Reg. No. IMC/BIR/15/67588 kilichotolewa na Institute of Finance Management (IFM) Dar es salaam mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Control No. 9910833882712.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MAYALA FAIDA MCHONGA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajiri **MC 4740 DCL.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya Polisi

**PHQ/SIN/MAN/5373/2024**

**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA**
**Kituo cha MPINDO Mkoa SIMIYU**
**Shauri la Madai/ Ndoa Na. 07/2024**
**Jina la mdai ............IGOLA MGUNGUHYA**
**Jina la mdaiwa.............YOHANA MAKUBI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa YOHANA MAKUBI WA IPILILO**
**MASWA**
**K.K AFISA MTENDAJI**
**KIJIJI CHA IPILILO**
**MASWA**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**(Eleza hapa habari za madai)**

**ANADAI KURUDISHIWA MAHARI YAKE NG'OMBE SITA (6)**

Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 20 mwezi 09 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 09 mwaka 2024

## KUPOTEA KWA CHETI



**SWAUM RAMADHANI JUMANNE** anatangaza kupotea kwa cheti cha Tanzania Public Service College (TPSC) kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Chuo cha Utumishi wa Umma Singida mwaka 2014. Kwa yeyote atakayekiona atoe Taarifa kituo chochote cha polisi **PHQ/SIN/SIN/7434/2024.**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO. 21951 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**DISMAS MATHAYO MNKUNDE**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY SLYVESTER MATEW MNKUNDE**

**GENERL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSON** Claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 30th day of September 2024

Dated at Korogwe this 09th day of September 2024

## KUPOTEA KWA BAJAJI

**VICTORINA MSARU NTANDU**

anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji yenye usajili namba MC 601 DDH. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/NJO/WAN/4086/2024**


## KUPOTEA KWA VYETI



**SHANGWE ISAYA KAAYA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NO S5263-0026 -2021 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI NOVEMBER 2021 NEEMAH SECONDARY SCHOOL. NA CHA DARASA LA SABA KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI MWAKA 2017 KATIKA SHULE YA SING'ISI CHENYE NAMBA PS0105083-104

KWA YEYOTE ATAKAYEVIONA ATOE TAARIFA POLISI **.**
**PHQ/PWA/KIB/18747/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GIDION ALOYCE JOSEPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S4576-0038** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **PAROMA SECONDARY** mwaka **2020.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/ARU/ARU/33429/2024.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na.35/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SEVERIN ANTHONY SAMWEL wa CHANG'OMBE-DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA PASCAL SEVERINE ANTHONY**

**KWA : YOYOTE ANAE HUSIKA**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 30 Mwezi 09 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 12 Mwezi 09 Mwaka 2024.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 1463/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SELEMANI SALIM WENDO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA NA ISSA WENDO**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**


Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 07 mwezi 10 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetokewa leo tarehe 17 mwezi 09 mwaka 2024.

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA**
**Kituo cha DODOMA MJINI Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na. 318/2024**
**JINA LA MDAI ........... 1. SAMWEL SETH LUAGO 2. COLLETHE NZAWA KAZIMIRY**
**JINA LA MDAIWA .................. RASHID HAMZA SHEMKAMBI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**KWA**
**RASHID HAMZA SHEMKAMBI - DODOMA MJINI**
**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA SHILINGI 28,000,000/=**


Kwa hiyo unatakiwakuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 24 mwezi 09 mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi, kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima keleta shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajil iya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 Mwezi 09 Mwaka 2024.

## KUPOTEA KWA CHETI




**ABDALLAH OMARY NZUMILA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo chenye usajili namba **E0526-0079** kilichotolewa na **PATANDI TEACHERS' COLLEGE** mwaka **2021.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/200064/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MASETHO BATISTA MTANDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha **BACHELOR OF ARTS WITH EDUCATION** chenye usajili namba **BAED 48726** kilichotolewa na **THE SAINT AGUSTINE UNIVERSITY OF TANZANIA** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: PWA/BAG/RB/148312/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NURU TWAHA MWIFUNYI** anatangaza kupoteza cheti cha kumaliza kidato cha nne (4) chenye Index **NO,S 0909/013/2001** cha Shule ya Sekondari ya **NAZARENE** cha mwaka, kilichotolewa na **BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA)** Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi: **Taarifa ya Polisi ,PHQ/MBE/MBE/27846/2024**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Tani 2,955 za msaada kupelekwa Sudan

**ANKARA,** Uturuki

MELI iliyobeba tani 2,955 za misaada ya kibinadamu, iliyoandaliwa chini ya uongozi wa Mamlaka ya Kukabiliana na Maafa na Dharura (AFAD), imetumwa kutoka Bandari ya Kimataifa ya Mersin kuelekea Sudan.

Ilielezwa kuwa msaada wa kibinadamu umeanza kupelekwa rasmi nchini Sudan kwa uratibu wa AFAD, jimbo la Mersin, Wizara ya Mambo ya Nje, Hilali Nyekundu ya Uturuki na mashirika 12 yasiyo ya kiserikali.

Ilibainishwa kuwa misaada hiyo ni pamoja na chakula, vifaa vya usafi na afya, malazi, pamoja na jenereta, mahema na duka la kuoka mikate, zilipakiwa kwenye meli hiyo na kupelekwa nchini Sudan.

Akizungumza katika hafla ya kuaga bandarini hapo jana, Makamu wa Rais wa AFAD Hamza Tasdelen, alisema wanatarajia pia kutuma meli ya pili ya msaada nchini Sudan.

"Leo (jana) tumekusanyika hapa kutuma karibu tani 3,000 za msaada, hii ni pamoja na mahema 18,500, mablanketi zaidi ya 17,000 na vifaa mbalimbali vya makazi, tani 1,000 za unga na karibu tani 500 za paket za chakula," alisema.

Tasdelen aliongeza kuwa meli ya kwanza waliyotuma kutoka Mersin iliwasili Sudan Julai 19 ikiwa na tani 2,500 za misaada ya kibinadamu akibainisha kuwa kuna matatizo katika eneo karibu na Turkiye, ikiwa ni pamoja na migogoro ya ndani inayoendelea, ukame na mvua nyingi nchini Sudan.

Akiangazia juhudi zinazofanywa kusaidia Sudan, Tasdelen alisema "Nchi yetu inaendelea kusimama pamoja na wanadamu wote, bila kujali dini, lugha, au rangi duniani kote."

"Tunatanguliza shukrani zetu za dhati kwa mashirika yetu yasiyo ya kiserikali na Hilali Nyekundu ya Uturuki. Kama kawaida, tulitayarisha maudhui ya misaada pamoja kwa meli hii pia," alisema.

"Hii si mara ya kwanza sisi kufanya hivi, hiyo ni meli ya 14 tumetuma kwa mwaka huu, kumi na wawili kati yao walitumwa Misri kwa ajili ya kupelekwa Gaza, pia tumetoa misaada muhimu huko, kwa sasa tumetuma jumla ya tani 75,000 za nyenzo kwa Gaza," alisema.

Tasdelen alisisitiza kuwa chini ya uongozi wa Rais Recep Tayyip Erdogan na maagizo ya Waziri wa Mambo ya Ndani Ali Yerlikaya, uamuzi umefanywa wa kufikisha tani 30,000 za unga huko Gaza mwaka huu.

Alieleza kuwa watapeleka unga huko Gaza kwa jumla ya shehena tisa, na kwamba kufikia Septemba 13, wamekamilisha usafirishaji wa tano, akieleza kuwa watasafirisha zingine nne kila baada ya siku 10.

**TRT**

# Biden akemea jaribio la mauaji ya Trump

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Joe Biden, amekemea jaribio la pili la mauaji dhidi ya mtangulizi na mpinzani wake kisiasa Donald Trump, na kulaani ghasia hizo za kisiasa kuwa sio tabia za Marekani.

Akizungumza wakati wa mkutano wa vyuo vikuu na vyuo vikuu vya watu weusi (HBCU), akiwa mjini Philadelphia juzi, Rais Biden alisema hakuna mahali pa kufanya vurugu za kisiasa katika taifa hilo.

Alisema ndani ya Marekani, kuna usuluhishaji wa tofauti zao kwa amani na kutumia sanduku la kura, lakini sio wa mtutu wa bunduki. akisisitiza kwamba taifa hilo liliteseka mara nyingi na mikasa ya mauaji ya bunduki na kwamba njia hiyo haisuluhishi chochote zaidi ya kusambaratisha nchi.

Maoni ya Biden yametolewa takriban saa 24 baada ya maofisa wa idara ya ulinzi wa viongozi ya Marekani, kumwona mtu anayeshukiwa kuwa na bunduki kwenye uwanja wa gofu wa Rais mstaafu Donald Trump, West Palm Beach, Florida.

Ilielezwa kuwa mtu huyo mwenye bunduki alijificha kwa takriban saa 12 vichakani kabla ya Donald Trump kucheza mchezo ambao haukuwa umepangwa wa gofu katika klabu yake iliyopo kando ya bahari huko Florida.

Ilielezwa kuwa tukio hilo liliwaacha wengi wakiwa na mshangao kwa kile maofisa wanasema linaonekana kuwa jaribio la pili la kumuua rais huyo wa zamani katika muda wa miezi mingi.

Hata hivyo, baada ya jaribio hilo, Trump alikimbizwa hadi kwenye eneo salama, na kwamba tukio hilo limetokea miezi miwili tu baada ya jaribio lingine la mauaji dhidi yake huko Butler, Pennsylvania, ambako Trump alipigwa risasi sikioni wakati wa mkutano wa kufanya kampeni.

**VOA, BBC**



Hali ya wananchi ilivyo katika kambi inayoendeshwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) katika mji wa mpaka wa Sudani wa Gallabat. **PICHA: AFP**

# Mataifa yanayoongozwa kijeshi kutengeneza pasipoti zao mpya

**BAMAKO,** Mali

NCHI tatu za Afrika Magharibi zinazoongozwa na tawala za kijeshi zinatarajia kuzindua pasipoti mpya za kibayometriki katika siku zijazo kama sehemu ya kujiondoa kutoka kwa umoja wa kikanda wa Ecowas.

Mali, Burkina Faso na Niger, ambazo viongozi wake wa kijeshi walichukua madaraka katika mfululizo wa mapinduzi kati ya 2020 na 2023, walitangaza mpango wao wa kuondoka kwenye umoja huo Januari mwaka huu.

Kutokana na mapinduzi hayo, nchi za Afrika Magharibi ziliwawekea vikwazo wanajeshi hao, zikilenga kuwasukuma kurejesha utawala wa kiraia haraka, jambo ambalo halikuonekana kuleta matokeo kwa haraka.

Ilielezwa kuwa mataifa hayo matatu ambayo sasa yanaunda Muungano wa Nchi za Sahel hadi sasa yamepinga wito huo, yakiamua kuimarisha muungano wao.

"Katika siku zijazo, pasipoti mpya ya kibayometriki ya muungano itasambazwa kwa lengo la kuunganisha hati za kusafiria katika eneo letu la pamoja," kiongozi wa serikali ya Mali Kanali Assimi Goita alisema katika hotuba yake ya televisheni.

Kanali Goita, ambaye ni kaimu rais wa muungano wa Sahel, alizungumza siku moja kabla ya serikali za kijeshi kuadhimisha mwaka wa kwanza tangu wafanye uamuzi wa kuunda muungano wao wenyewe.

Alisema pia walikuwa wakipanga kuzindua huduma ya pamoja ambayo itakuza usambazaji wa habari kwa usawa katika mataifa yote matatu.

Ilielezwa kuwa Burkina Faso ilikuwa imefichua mapema uamuzi wake wa kuzindua pasipoti mpya ya kibayometriki bila nembo ya Ecowas.

Hata hivyo, bado haijulikani jinsi pasi hizo mpya za kusafiria zitaathiri usafiri wa raia wao kwenda mataifa mengine ya Ecowas ambako walifurahia kusafiri bila visa kama wamiliki wa pasipoti ya kikanda ya mataifa 15.

Mwezi Julai, wakuu wa serikali walisema walikuwa wameshaamua kuhusu uamuzi wao huku wakiipa kisogo Ecowas. Na kwamba wanataka kujenga jumuiya ya watu huru kwa kuzingatia maadili ya Kiafrika na mbali na udhibiti wa mataifa ya kigeni.

Tangazo la hivi punde linakuja wakati Ecowas inajishughulisha na juhudi za kuyafanya mataifa matatu ya Sahel kurejea katika umoja huo, huku ikionya kuwa kurasimishwa kwa kundi lililojitenga kulileta hatari ya kusambaratika kwa eneo hilo na kuzidisha ukosefu wa usalama.

**BBC**

# KOCHA KENGOLD AACHIA NGAZI, MKUU WA MKOA ATOA ANGALIZO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Kocha Mkuu wa KenGold, Fikiri Elias, amejiuzulu kuifundisha timu hiyo kutokana na matokeo mabovu, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewataka viongozi wa klabu hiyo kujitathmini, kuangalia wapi wanakwama, ikiwezekana dirisha dogo wafanye usajili mkubwa.

Akizungumza jijini Mbeya jana, Homera alisema Ligi Kuu Tanzania Bara si lelemama, hivyo viongozi wa klabu hiyo wanatakiwa kuangalia kitu gani wafanye ili kuiondoa timu hiyo kwenye vipigo mfululizo ambavyo vinaifanya kuwa katika hatari ya kurejea Ligi ya Championship.

Haya yanatokea baada ya timu hiyo kupata kipigo cha bao 1-0 juzi, Uwanja wa KMC Complex uliopo Mwenge, Dar es Salaam kikiwa ni cha tatu mfululizo kwenye Ligi Kuu.

Awali ilifungwa mabao 3-1 dhidi ya Singida Black Stars na mabao 2-1 dhidi ya Fountain Gate.

"KenGold wajipange, wasifikiri Ligi Kuu ni kama Daraja la Kwanza (Championship), kule ni vita na fitina juu, kwa hiyo viongozi wapate salamu hizi kuwa Ligi Kuu si lelemama, tunajenga Uwanja wa Chunya kupitia mapato ya ndani kushirikiana na wadau wa Chunya kwa ajili yenu, lakini mjitathmini, mjipange," alisema mkuu wa mkoa huyo.

Alisema timu hiyo ni lazima isajili wachezaji wazoefu kwenye Ligi Kuu kwani inavyoonekana haina wachezaji wa aina hiyo.

"Timu ni lazima iwe na wachezaji wenye uzoefu mkubwa na wapambanaji, mwambieni mmiliki wa timu bila kuwa na kikosi imara itarudi Championship, kitu ambacho sisi hatukitaki, kwa hiyo dirisha dogo kama ana uwezo wa kumsajili Maxi Nzengeli, au Stephane Aziz Ki, awalete hapa," alisema Homera.

Wakati mkuu wa mkoa huyo akisema hayo, Kocha Fikiri Elias amejiuluzu kuifundisha timu hiyo kwa kile alichodai kushindwa kutimiza malengo yake.

Kocha huyo amejiuzulu pamoja na msaidizi wake, Luhanga Makunja, walijiuzulu juzi baada ya kipigo dhidi ya KMC.

"Nilijiwekea malengo kuwa nisipopata pointi sita katika michezo minne basi nitajiuluzu, sasa tayari mchezo wa tatu hatujapata pointi hata moja, na hata kama nikiendelea na kushinda tunakuwa na pointi tatu. Mimi kama mwana taaluma, nimefanya hivi kulinda taaluma yangu pamoja na uwajibikaji," alisema kocha huyo.

Taarifa ya klabu hiyo iliyopanda daraja kuanza kucheza Ligi Kuu msimu huu, imesema kuwa imekubali makocha hao kujiuzulu na kikosi kwa sasa kitakuwa chini ya kocha wa zamani wa timu hiyo aliyeipandisha daraja, Jumanne Chale.

## Tamasha kuichangia Mwananyamala laiva

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha afya ya jamii nchini inazidi kuimarika, Gym ya JK Mzungu Fitness, imeandaa tamasha maalum litakalofanyika Oktoba 19, mwaka huu, kwenye Fukwe za Msasani, Dar es Salaam, likiwa na lengo la kukusanya fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya wodi ya wazazi kwenye Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mmiliki wa Gym ya JK Mzungu Fitness, Janeth Kimambo, alisema kaulimbiu ya tamasha hilo ni ‚Afya ya Mama ni Afya ya Familia' na kwamba wameamua kuandaa tamasha hilo kutokana na kutambua thamani ya mama na mtoto katika familia.

"Tumechagua hospitali hii kwa kuwa tunatambua thamani ya mama na mtoto kwa kuwasaidia kununua vifaa ambavyo vitawasaidia wanawake wajawazito pamoja na watoto," alisema Kimambo.

Alisema tamasha hilo litashirikisha michezo mbalimbali ikiwamo riadha na kuweka wazi washiriki watapata fursa ya kupima presha, sukari pamoja na kupewa ushauri kutoka kwa madaktari bingwa wa hospitali hiyo.

Alitoa wito kwa taasisi nyingine kuwaunga mkono ili waweze kufanikisha tukio hilo, lakini pia akiwata Watanzania kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi kwa bidii kwa kuwa yanajenga afya zao.

Kwa upande wake daktari bingwa wa magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi hospitalini hapo, Luzango Maembe, alisema anaishukuru gym hiyo kwa kuamua kuwasaidia kununua vifaa hivyo ambavyo vitapunguza vifo vya mama mjamzito pamoja na watoto.

Katika hatua nyingine, Kiongozi wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Filex Chunga, alisema siku hiyo kutakuwa na mbio za kilometa tano na 10.

## Inter Z'bar FC yalia na ugeni Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Inter Zanzibar FC, imesema uwanagenzi wao katika Ligi Kuu Zanzibar ndio kitu pekee kinachowatesa na kushindwa kupata matokeo mazuri.

Inter Zanzibar FC imejikuta ikipoteza mchezo wao wa pili wa ligi hiyo baada ya kukubali kichapo cha mabao 4-0 kutoka kwa wakongwe wa soka, Malindi SC, mchezo uliochezwa juzi katika Uwanja wa New Amaan Complex, visiwani hapa.

Mpaka sasa tayari Inter Zanzibar imepoteza michezo miwili mfululizo ya ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar, PBZ.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumalizika mchezo wake wa pili Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Faki Abdi, alisema si kama wanakikosi kibaya ila bado wachezaji wake hawajaweza kuzisoma mbinu za wapinzani wao hasa pale wanapocheza na timu zenye uzoefu katika ligi hiyo.

"Wachezji wanapambana sana uwanjani, lakini bado uwanagenzi wetu ndio unatutesa, lakini bado tunamatumaini ya kubadilika na kucheza vizuri,"alisema.

CHAMBUA...



Mchezaji wa timu ya soka ya Bulls, Said Mbinga (katikati), akijaribu kuwapangua wachezaji wa timu ya soka ya Mtoni Sabasaba Sports Center, walipokutana kwenye mchezo wa kirafiki katika Uwanja wa Gymkhana, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Viungo, mastraika tatizo Kagera Sugar - Kocha

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Kagera Sugar, Mganda, Paul Nkata, amesema katika kikosi chake shida kubwa ni viungo washambuliaji na mastraika, ambao ndio wamesababisha kufikisha mechi nne kwenye Ligi Kuu bila kufunga hata bao moja.

Akizungumza juzi baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya JKT Tanzania uliopigwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, timu hizo zikitoka suluhu, kocha Nkata alisema viungo washambuliaji wake wamekuwa hawatengenezi nafasi nyingi, lakini pia hata hizo chache zinazopatikana, mastraika nao wamekuwa wakimwangusha kwa kukosa mabao.

"Leo tulihitaji kushinda, lakini kwa bahati mbaya tumepata moja, mechi ya nne hatujafunga hata bao moja, shida hapa inaonekana viungo wetu na washambuliaji ni tatizo.

Hebu angalia, hata nafasi chache zilizopatikana, lakini utulivu unakosekana kwa mastraika, nadhani labda mechi zinazofuata tutarekebisha tuone nini tunafanya ili tufunge mabao na kupata matokeo mazuri," alisema.

Alisema alijiunga kwenye kikosi hicho akiwa amechelewa, hivyo ameshindwa kujua mchezaji gani ana kiwango gani kushinda mwingine, jambo ambalo limemfanya kuwapanga kutokana na kile tu anachokiona mazoezini, lakini kwa sasa angalau ameanza kujua ni wachezaji gani wana viwango vinavyoweza kuisaidia timu.

Hata hivyo, zipo taarifa kuwa kocha huyo amepewa michezo kadhaa ambapo kama hatofanya vizuri anaweza kutimuliwa.

Kagera, imecheza mechi nne, ikiwa haijashinda hata moja, ikitoka sare moja na kupoteza mitatu, haijafunga bao, ikiruhusu manne, ina pointi moja ikiwa kwenye nafasi ya 14 ya msimamo wa Ligi Kuu.

Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema dakika 15 za kwanza hawakuanza vizuri, lakini baadaye wakaushika mchezo.

"Tuliwasoma kwenye michezo yao miwili iliyopita, tuliwakamata, ni kwamba hatukutumia tu nafasi tulizozipata, lakini hii imeisha kwa sasa tunajiandaa na mechi dhidi ya KMC," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GOMES ATAKIWA LIVERPOOL
LIVERPOOL imeripotiwa kutaka kumsajili kiungo wa kati wa Lille, Angel Gomes, huku maskauti wa 'Wekundu' hao wakihudhuria mchezo wa kwanza wa kuvutia wa mchezaji huyo wa kwanza wa England dhidi ya Finland mwezi huu. (***Liverpool Echo***)

### CHILWELL AFUATILIWA PALACE
KLABU za Crystal Palace na Ipswich zote zinamfuatilia beki wa kushoto wa England na Chelsea, Ben Chilwell, kabla ya uhamisho wa Januari. (***Sun***)

### MUSIALA NA BAYERN
KLABU ya Bayern Munich inatatizika kumshawishi kiungo mkabaji Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 21, kuongeza mkataba wake na klabu hiyo, jambo ambalo linaweza kuibua nia ya kumnunua mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ujerumani kutoka Manchester City na Manchester United. (***Daily Mirror***)

### POPE AWINDWA EVERTON
KOCHA wa Everton, Sean Dyche, anafikiria kumnunua kipa wa England na Newcastle United, Nick Pope, mwenye umri wa miaka 32, kuchukua nafasi ya Jordan Pickford, 30. (***Daily Mirror***)

### RABIOT ANUKIA MARSEILLE
KIUNGO wa kati wa zamani wa Juventus, Adrien Rabiot, ambaye ni mchezaji huru, anakaribia kujiunga na klabu ya Ligue 1 ya Marseille baada ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 29, kuhusishwa na Klabu za West Ham na Manchester United. (***L'Equipe***)

### DIALLO MKATABA MPYA
KLABU ya Manchester United inatarajiwa kumpa winga Amad Diallo mwenye umri wa miaka 22, mkataba mpya wa muda mrefu katika miezi ijayo. Mkataba wa sasa wa raia huyo wa Ivory Coast unamalizika msimu huu wa majira ya joto. (***Manchester Evening News***)

### GERRARD KUREJEA RANGERS
MLANGO unaweza kuwa wazi kwa bosi wa zamani, Steven Gerrard, kurejea Rangers na kuchukua nafasi ya Philippe Clement kama kocha. (***Daily Record***)

### WHITE AFUATILIWA CITY
MANCHESTER City inamfuatilia kiungo wa Nottingham Forest, Morgan Gibbs-White mwenye umri wa miaka 24, lakini Forest wana nia ya kumpa mchezaji huyo wa Kimataifa wa England mkataba mpya. (***HITC***)

### MENDY KUSAINI MADRID
MLINZI wa kushoto wa Real Madrid na Ufaransa, Ferland Mendy mwenye umri wa miaka 29, anatazamiwa kusaini mkataba mpya na klabu hiyo ya Hispania hadi 2027. (***Marca***)

### ZOUMA KWA MKOPO
MLINZI wa West Ham Mfaransa Kurt Zouma mwenye umri wa miaka 29, amekamilisha uchunguzi wa matibabu na anakaribia kukamilisha uhamisho wa awali wa mkopo kwenda kwa Al-Orouba ya Saudi Pro League. (***Sky Sports***)

### ARAUJO AULIZIWA CHELSEA
CHELSEA imemuuliza beki wa Benfica, Mreno Tomas Araujo mwenye umri wa miaka 22. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL HAITISHWI KIWANGO CHA HAALAND – JORGINHO

**LONDON,** England

WACHEZAJI wa Arsenal hawajashtushwa na kiwango cha mshambuliaji wa Manchester City, Erling Haaland, cha kufunga mabao, kiungo wa kati Jorginho alisema akithibitisha kujiamini kwa timu hiyo ya Kaskazini mwa London kabla ya mechi ya Jumapili ya Ligi Kuu dhidi ya City.

City wamekuwa na kampeni nzuri katika ligi hadi sasa, huku Arsenal wakishinda mara tatu na sare moja.

**Akiwa na mabao tisa katika michezo minne ya ligi, ikijumuishwa na hat-trick mbili, Haaland amefunga mabao 99 katika mechi 103 alizoichezea City kwenye mashindano yote.**

Mshambuliaji huyo wa Norway atalenga kwa karne yake kwenye mpambano wa leo Jumatano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Inter Milan, huku Arsenal wakianza kampeni yao ya Ulaya na huko Atalanta Alhamisi na kujiandaa kukutana na City pale Etihad Jumapili.

> ●●● Kila mtu anataka kuimarika na anataka kuwa bora kwa timu, ni vizuri kuamini unachofanya, tuko kwenye njia...

"Erling akifunga tena ... inaanza kutuchekesha," alisema Muitaliano huyo mwenye umri wa miaka 32.

"Tunaangalia kwa sababu tunatazama michezo yote na tunapenda Ligi Kuu."

"Tunatazama City pia, ambayo ni ya kawaida. Haitufikii kichwani. Tunahitaji kuangazia sisi na hilo ndilo tunalojaribu kufanya."

Jorginho alisifu mawazo ya Arsenal, akisema imeimarika tangu msimu uliopita, akiashiria ushindi wao wa bao 1-0 dhidi ya Tottenham Hotspur licha ya kuwakosa wachezaji muhimu kama nahodha Martin Ødegaard na Declan Rice.

"Unajifunza zaidi kuhusu kila mmoja ... kila mtu anataka kuimarika na anataka kuwa bora kwa timu. Unapoiweka timu katika nafasi ya kwanza nadhani mambo mazuri yanaweza kutokea," aliongeza.

"Endelea kuamini unachofanya, nadhani tuko kwenye njia sahihi."

Arsenal walimaliza ligi wakiwa nafasi ya pili msimu uliopita, kwa kupata ushindi wa bao 1-0 nyumbani na kutoka suluhu wakiwa ugenini katika mechi zao za ligi na City.

## HABARI MICHEZO




# ROMERO NA MAUMIVU KICHAPO SPURS

**LONDON,** England

MLINZI wa Tottenham Hotspur, Cristian Romero, alionekana kukerwa na maandalizi ya klabu hiyo kwa kushindwa na Arsenal Jumapili katika chapisho lililosambazwa kwenye mitandao ya kijamii.

Romero alicheza kwa dakika 90 kwenye mchezo huo mgumu, ambao Spurs walionekana kutawala kwenye karatasi za takwimu, lakini hawakufanikiwa kupata bao, ila hakuweza kuzuia bao la kichwa la Gabriel kipindi cha pili kuwapa Arsenal pointi zote tatu.

Baada ya mchezo huo, Romero alionekana akishiriki chapisho kwenye mtandao wa X, ambao zamani ulijulikana kwa jina la Twitter, na mwandishi wa habari wa Argentina, Gaston Edul, ambayo ilitilia shaka maandalizi ya Tottenham kwa mchezo huo.

“Tottenham ilishindwa tena na Arsenal,“ aliandika. „Haikuja kupigana, lakini maelezo zaidi: Ilikuwa ni klabu pekee ya Ligi Kuu iliyowarudisha wachezaji wake kutoka kwa timu zao za kitaifa peke yao na bila mipango kutoka kwa klabu, kama ilivyoamuliwa na wasimamizi.

“Hiyo iliipa Arsenal faida kwa sababu wachezaji wao walifika wakiwa wamepumzika kidogo kuliko wapinzani.“

# Ten Hag amtaka Antony kupambania namba

**MANCHESTER,** England

ANTONY lazima „apambane“ ili kushinda tena nafasi yake katika timu ya Manchester United, kwa mujibu wa kocha Erik ten Hag.

Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Brazil ni uhamisho wa pili ghali zaidi katika historia ya United baada ya kuwasili kutoka Ajax kwa mkataba wa pauni milioni 82 mwaka 2022.

Lakini amekuwa hana nafasi pale Old Trafford na alicheza kwa dakika moja tu kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Hata hivyo, Mholanzi huyo alisisitiza kwamba Antony hatacheza isipokuwa anastahili kupambania nafasi.

“Tutaona itakuwaje,“ alisema Ten Hag alipoulizwa kama Antony anaweza kukabidhiwa mwanzo wake wa kwanza wa msimu.

“Tunafanya mazoezi kila siku na wachezaji wanapaswa kupata haki. Mtazamo unapokuwa mzuri na wanaonesha uchezaji mazoezini basi watacheza.”

Luke Shaw anasalia nje ya uwanja kwa sababu ya tatizo la kucheza na kocha huyo amekataa kuweka muda wa kurejea kwa beki huyo wa pembeni.

“Anaendelea vema,“ Ten Hag alisema.

“Ni kweli tuna mpango kichwani wakati anaweza kuwa tayari, lakini siku zote unategemea maendeleo yatakwendaje na huwezi kutoa pendekezo kwa sababu kuna mambo mengi, mpango unaweza kuongeza kasi au kupunguza kasi.”





# Barca yakataa dau la mamilioni kumuuza Yamal

**BARCELONA,** Hispania

WAKALA wa kiungo wa kati wa Barcelona, Dani Olmo, amethibitisha kuwa timu hiyo ya Hispania ilikataa ofa iliyoweka rekodi ya dunia kutoka kwa Paris Saint-Germain kwa ajili ya winga, Lamine Yamal.

Iliripotiwa mapema msimu wa majira ya joto kuwa PSG, katika kutafuta mbadala wa Kylian Mbappe, walipendekeza dili la thamani ya euro milioni 250 ili kumsajili winga huyo siku chache kabla ya siku yake ya kuzaliwa ya kutimiza umri wa miaka 17.



Sakata hilo liliisha ghafla kama lilivyoanza, huku Barcelona wakiripotiwa kurudisha ofa hiyo haraka sana, huku mashabiki wengi wakihoji iwapo dau la PSG lipo kweli.

"Jambo moja ninalojua kwa uhakika ni kwamba Barcelona walikataa ofa kubwa kwa Lamine Yamal kutoka PSG miezi kadhaa iliyopita,“ alisema wakala Andy Bara akiiambia Podcast Inkubator.

"Mkataba huo ulikuwa na thamani ya karibu euro milioni 250.“

Bara, ambaye pia anawakilisha wachezaji kama Nacho Fernandez na Mikayil Faye, aliendelea kujadili uhamisho wa Olmo kwenda Barcelona msimu huu wa majira ya joto.

Barcelona ililazimika kufanya kazi kwa bidii kutafuta fedha za kumsajili Olmo, ambaye alilazimika kusubiri wiki mbili kabla ya klabu hiyo kumudu kumsajili kwenye kikosi chao cha LaLiga, lakini Bara alisisitiza Olmo hakuwahi kuwa na mashaka yoyote juu ya kufanya mabadiliko hayo.

"Vyombo vya habari vilipiga kelele nyingi, lakini Rais Joan Laporta aliniambia nisiwe na wasiwasi na kwamba baada ya siku 15 itasuluhishwa kama ilivyotokea,“ Bara alieleza.

# HABARI MICHEZO

## Rais CAF atoa kauli mechi Simba Libya

INATOKA UKURASA 24

mawili, kimoja kikipitia nchini Uturuki na kingine Cairo nchini Misri.

Ahmed, alisema kuwa Kocha Mkuu, Fadlu Davids, amemwambia kuwa kwa sasa anaandaa mfumo na mbinu za kushambulia baada ya mfumo wa kwanza kufanikiwa.

"Kila kitu kinakwenda sawa, hatuna majeruhi na wote wako tayari kwa mchezo unaofuata. Mechi bado ni ngumu na haijaisha ndiyo maana tunaendelea kujiandaa ili kushinda na kwenda hatua ya makundi.

"Fadlu amejiandaa na mbinu na mfumo wa kucheza nyumbani, mechi iliyopita ilikiwa ni mbinu ya kucheza ugenini kuhakikisha hatupotezi na hilo limefanikiwa, kwa sasa anaandaa mpango madhubuti kuhakikisha tunapata ushindi, katika mechi ya marudiano linatakiwa jambo moja tu ni ushindi, sare haitusaidii, kitu pekee kitakachotuvusha ni ushindi," alisema.

## Gamondi apania 'gharika' kwa ...

INATOKA UKURASA 24

kuandaa mbinu za pamoja, lakini sasa amepata muda wa kuwa na kikosi chake chote.

Kwa upande wa Meneja wa Klabu hiyo, Walter Harrison, alisema malengo yao ni kufanya vema kwenye mchezo wao wa marudiano ili waweze kuingia hatua ya makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Kwa sasa tunaendelea kuwajenga kisaikolojia wachezaji wetu ili tuweze kupata pointi tatu katika mchezo wetu huo, uwanja ambao tutakwenda kuutumia tunaufahamu kwa kuwa tulishawahi kuutumia," alisema Harrison.

Katika hatua nyingine, Ofisa Habari wa Klabu ya Yanga, Ali Kamwe, amesema kikosi cha Yanga kitanarajia kuondoka jijini Dar es Salaam kesho kuelekea Zanzibar, huku kile cha CBE nacho kikitarajiwa kutua siku hiyo na kuunganisha moja kwa moja kwa boti kuelekea Zenji, ambapo huenda wakakutana bandarini, Dar es Salaam.

Kwa maana hiyo huenda timu hizo zikasafiri pamoja kesho kuelekea kwenye mchezo huo ambao utapigwa saa 2:30 usiku kwenye Uwanja wa New Amaan, Zanzibar baada ya mchezo wa kwanza uliopigwa, Uwanja wa Abebe Bikila, Jumamosi iliyopita, Yanga kupata ushindi wa bao 1-0.

# GOFU WANAWAKE YAHITIMISHWA ARUSHA NBC IKIAHIDI MAZURI ZAIDI

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MASHINDANO ya siku tatu ya Gofu yajulikanayo kama Tanzania Ladies Open Golf Tournament, yamehitimishwa mwishoni mwa wiki jijini Arusha huku wadhamini wakuu wa mashindano hayo, Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), wakiahidi kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuyaongozea ubora na ushindani utakaowavutia washiriki wengi kutoka ndani na nje ya nchi.

Mashindano hayo ya siku tatu yaliyofanyika kwenye viwanja vya Klabu ya Gofu ya Gymkhana jijini Arusha, yalifanikiwa kuvutia washiriki kutoka klabu zote za mchezo huo hapa nchini sambamba na washiriki wengine kutoka katika mataifa ya Kenya na Uganda huku mchezaji Mkenya Mercy Nyanchama akiibuka mshindi wa jumla.

Akizungumza kwenye hafla fupi ya kukabidhi zawadi kwa washindi mbalimbali wa mashindano hayo, Meneja Mahusiano wa Benki ya NBC, Gerald Tarimo, pamoja na kuwapongeza washiriki na washindi mbalimbali wa mashindano hayo, alisema benki hiyo itaendelea kuyaunga mkono ikiwamo kuyaboresha zaidi ikiwa ni sehemu ya jitihada zake katika kuchochea ushiriki wa wanawake katika michezo.

"Pamoja na kuvutiwa na idadi kubwa ya washiriki kwenye mashindano haya, zaidi tumevutiwa na maandalizi mazuri yaliyochochea ushindani uliokusudiwa kwa kuwa washiriki hawakuwa na changamoto ambazo zingeweza kuathiri uwezo wao kimchezo.

"Mara nyingi NBC tumekuwa tukikabidhi zawadi mbalimbali kwa washindi wa kiume zikiwamo klabu za mpira wa miguu kwenye ligi tatu tunazozidhamini nchini ikiwamo Ligi Kuu ya NBC, hivyo tunapopata nafasi ya kufurahia na kukabidhi zawadi kwa washindi wanawake kama leo hivi kwetu ni furaha pia," alisema.

Kwa mujibu wa Tarimo, kutokana na mafanikio yanayoendelea kuonekana kupitia udhamini wa benki hiyo kwenye mchezo wa gofu nchini, NBC inadhamiria kuendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa mchezo huo kufanikisha mashindano mbalimbali kwa viwango vyenye ubora zaidi ili kuchochea ukuaji na kuibua vipaji vipya hususan kwa watoto.

Kwa upande wa rais wa Chama cha Gofu cha Wanawake Tanzania (TLGU), Queen Siraki, pamoja na kuwapongeza washiriki na washindi mbalimbali wa mashindano hayo wakiwamo wale waliotoka nje ya nchi, pia aliwashukuru wadau mbalimbali waliofanikisha mashindano ikiwa ni pamoja na mdhamini mkuu wa mashindano hayo Benki ya NBC.

Aidha, Siraki alitoa wito kwa jamii hususan wanawake kushiriki kwa wingi kwenye mchezo huo unaojiongezea umaarufu hapa nchini huku akiwasihi wapuuzie dhana iliyojengeka kwa muda mrefu kuwa mchezo wa gofu ni mahususi tu kwa watu wenye kipato kikubwa kwenye jamii au wanaume tu.

"Maandalizi mazuri yaliyohusisha pia zawadi nzuri na zenye viwango kama ilivyokuwa kwenye mashindano haya ndio chachu ya kuendelea kuvutia zaidi washiriki kutoka ndani na nje ya nchi na kwenye hilo tunawashukuru sana wadhamini wetu hususan Benki ya NBC. Ni matumaini yetu wataendelea kutuunga mkono zaidi mashindano yajayo kwa kuwa tunatazamia kuwa na mambo mazuri zaidi kutokana na mwamko mkubwa unaoendelea kushuhudiwa ukihusisha ongezeko kubwa la wachezaji na vipaji vipya vya mchezo huu," alisema.



Meneja Mahusiano wa Benki ya NBC, Gerald Tarimo (katikati), akiwa kwenye picha ya pamoja na baadhi ya washiriki na washindi wa mashindano ya gofu ya Tanzania Ladies Open Golf Tournament wakati wa hafla fupi ya kuhitimishwa kwa mashindano hayo ya siku tatu, mwishoni mwa juma jijini Arusha. Benki ya NBC ilikuwa mdhamini Mkuu wa mashindano hayo yaliyofanyika kwenye viwanja vya Klabu ya Gofu ya Gymkhana jijini Arusha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Azam yazitaka tatu za kwanza Simba

**Na Shufaa Lyimo**

KATIKA kuhakikisha inazipata pointi tatu za kwanza kwenye mchezo wa Ligi Kuu msimu huu Klabu ya Azam inaendelea kujifua vikali ikijiandaa na mechi yao ijayo dhidi ya Simba itakayopigwa Septemba 26, mwaka huu.

Tangu msimu wa Ligi Kuu 2024/25, uanze, Azam FC hajafanikiwa kuzoa alama zote tatu kwani katika michezo miwili iliyocheza yote imeambulia sare.

Akizungumza na Nipashe jana, Msemaji wa timu hiyo, Thabit Zakaria maarufu Zaka Zakazi, alisema malengo yao ni kutwaa ubingwa msimu huu kwa kufanya vizuri katika michezo yao yote ilisalia.

"Kwa sasa tunajiandaa na mchezo wetu ujao dhidi ya Simba, ni mchezo ambao unatarajiwa kuwa na upinzani mkubwa kutokana na aina ya timu tunayokutana nayo," alisema Zaka Zakazi.

Alisema kwa sasa kila mchezaji ana morali ya juu kuhakikisha wanapata matokeo katika mchezo wao huo na kuomba mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono.

Zaka Zakazi alifafanua kuwa licha ya msimu huu kuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa, watapambana ili waweze kuipa mafanikio timu yao hiyo.

"Msimu huu una ushindani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu, lakini tutapambana ili tupate nafasi ya kushiriki mashindano ya kimataifa kwa mara nyingine msimu ujao," alisema Msemaji huyo.

Alisema licha ya kutolewa kwenye mashindano ya kimataifa, bado hawajakata tamaa na badala yake wataendeleza ushindani ili msimu ujao waweze kushiriki tena.

Azam FC ambayo msimu huu ilikuwa ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilitolewa raundi ya awali na APR ya Rwanda kwa jumla ya mabao 2-1, baada ya kushinda bao 1-0 nyumbani na kwenda kukubali kulala kwa mabao 2-0 katika mechi ya marudiano ugenini.

# Michezo

Nipashe

Jumatano Septemba 18, 2024




Ten Hag amtaka Antony kupambania namba UKURASA 22




Rais wa CAF, Patrice Motsepe

# Rais CAF atoa kauli mechi Simba Libya

## ●●● Aagiza uchunguzi vurugu za Al Ahli Tripoli, asema hatakubali katika kipindi chake...

**Na Adam Fungamwango**

KABLA hata barua ya malalamiko ya Klabu ya Simba haijaanza kufanyiwa kazi, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), Patrice Motsepe, ameagiza kufanyika uchunguzi dhidi ya vurugu walizofanyiwa wachezaji na baadhi ya viongozi wa klabu hiyo nchini Libya Jumapili iliyopita, kabla, wakati wa mechi na baada ya kumalizika kwa mchezaji wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Al Ahli Tripoli nchini humo.

Akizungumza nchini Kenya juzi, Motsepe alisema akiwa kama rais kwenye kipindi chake cha kuwapo madarakani, hatoweza kuvumilia kuona timu kuna ambayo inaweza kukubaliwa kufanya vitendo vya vurugu ambavyo vinalishushia heshima soka la Afrika, hivyo kuamua kufanyika uchunguzi haraka.

Rais huyo alikuwa akijibu moja kati ya maswali ya waandishi waliokuwa kwenye Kikao cha Watendaji Wakuu wa CAF, kilichofanyika nchini Kenya, ambapo pamoja na mambo mengine, wanahabari walipata nafasi ya kumuuliza maswali rais huyo mwenye dhamana ya soka la Afrika.

Kwa mujibu wa mwandishi, Collins Okinyo, aliyehudhuria mkutano huo wa wanahabari na rais wa CAF, alisema awali Motsepe alikuwa haelewi nini kimetokea na baada ya kuambiwa hivyo, alionekana kushtuka.

"Kwanza alishtuka, inaonekana hakuwa anafahamu hilo, aliulizwa na mmoja wa waandishi hapa Kenya, halafu akaamuru mmoja wa watu wa CAF, Samson Adam, afanye uchunguzi wa tukio hilo ambalo linalishushia heshima soka la Afrika, amesema akiwa kama rais hakuna timu ambayo inaweza kukubaliwa kufanya vitendo vya vurugu," alisema mwandishi huyo.

Ingawa klabu hiyo haikutaka kuliweka hadharani jambo hilo, lakini taarifa kutoka ndani zinasema tayari wameshatuma malalamiko CAF ili wachukue hatua, kutokana na mashabiki wa klabu hiyo kufanya fujo kubwa kwenye Uwanja wa Juni 11 jijini Tripoli, wakati mechi ikiendelea na baada ya hapo.

Baadhi ya vyombo vya habari nchini humo na waandishi mbalimbali wa Afrika waliokuwapo katika mchezo huo, wamethibitisha klabu hiyo kushtaki juu ya vurugu iliyofanywa na wenyeji wao.

"Simba imeamua kutuma mlalamiko CAF dhidi ya Al Ahli Tripoli na hili limethibitishwa.

"Chupa za maji, vitu vya plastiki walirushiwa wachezaji na viongozi, lakini pia lugha mbaya, matusi, maneno ya kibaguzi na kushambuliwa kwa wachezaji na baadhi ya viongozi wa timu hiyo ya Tanzania vilitolewa, kabla na baada ya mechi yao iliyoisha kwa sare ya bila ya kufungana usiku wa Jumapili iliyopita.

"Viongozi wa Simba wamekusanya ushahidi wote uliopo na wameuwasilisha CAF ili kutafuta haki na adhabu dhidi ya upande wa klabu hiyo ya Libya," vyanzo mbalimbali vya habari viliandika.

Baada ya mchezo huo iliripotiwa viongozi na wachezaji walipigwa chupa za maji, ambapo hali ilikuwa mbaya uwanjani kiasi cha wachezaji kukimbizwa haraka vyumbani.

Meneja Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema wakiwa jukwaani, golikipa Aishi Manula alishambuliwa, huku mashabiki wa timu hiyo wakiendelea kufanya fujo uwanjani kwa saa kadhaa ambapo ililazimika wakae vyumbani hadi fujo zilipopungua.

Tayari kikosi cha Simba kimewasili alfajiri ya leo na kwenda moja kwa moja kambini tayari kwa mchezo wa marudiano utakaochezwa Jumapili ijayo, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kikosi hicho kimewasili kwa makundi

INAENDELEA UK. 23

## Gamondi apania 'gharika' kwa CBE

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA mchezo wa marudiano wa raundi ya kwanza wa Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema anaamini wachezaji wake watafanya vizuri Jumamosi kwa kufunga mabao mengi katika Uwanja wa New Amaan Complex, visiwani Zanzibar dhidi ya CBE ya Ethiopia kutokana na kufanyia marekebisho kasoro zilizojitokeza kwenye mechi ya awali.

Gamondi aliyasema hayo jana wakati alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari katika siku ya kukutana na vyombo vya habari, tukio ambalo lilifanyika makao makuu ya klabu hiyo yaliyopo mitaa ya Twiga na Jangwani jijini Dar es Salaam.

"Malengo yangu ni kuingia hatua ya makundi kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kuhakikisha tunafanya vizuri katika mchezo wetu wa Jumamosi," alisema.

Yanga inapigania kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa kwa mara ya pili mfululizo na mara ya tatu tangu kuanzwa kwa mfumo wa makundi.

Mara ya kwanza ilikuwa 1998, ambapo ilimaliza ikiwa ya mwisho kwenye kundi, msimu uliopita ilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali ilipotolewa na Mamelodi Sundows ya Afrika Kusini kwa mikwaju ya penalti 3-2 baada ya timu hizo kutoka suluhu katika michezo yote miwili wa kwanza ukianzia Dar es Salaam na wa pili ukichezwa, Afrika Kusini.

Gamondi alisema mchezo uliopita dhidi ya CBE wachezaji wake walicheza chini ya kiwango kwani walipata nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

"Mchezo uliopita mengi yalisemwa, lakini tunashukuru tulipata pointi tatu katika mchezo huo kwa sasa tunajipanga kwa ajili ya mechi yetu ya marudiano ambayo naamini itakuwa na ushindani mkubwa," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Aidha, alisema maandalizi ya mchezo uliopita yalikuwa na changamoto kutokana na wachezaji wake walikuwa kwenye timu za taifa, hivyo kukosa muda wa kutosha

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >